IBADA YA KILA SIKU

TOLEO LA 3

Jul-Ago-Sep 2021

# HabariNjema

## KILA SIKU

**BURE**

HAKIUZWI

KITABU HIKI CHA IBADA KIMESHALIPIWA NA WASHIRIKA WETU ILI KISAMBAZWE BURE

KAMA VILE MAJI YA BARIDI KWA MTU MWENYE KIU, NDIVYO ILIVYO HABARINJEMA ITOKAYO KATIKA NCHI YA MBALI. [MITHALI 25:25]

Uebert & BeBe ANGEL

GoodNews

Become a

# GoodNewsWorld PARTNER




PARTNER NOW AND HELP SPREAD
THE **GOODNEWS** AROUND THE WORLD

VISIT www.goodnewsworld.com/ partner




## UEBERT & BEBE ANGEL

Wakiwa na miaka mingi ya kufanya huduma ya Mungu, Uebert na Bebe Angel ni mapainia na sauti zinazoongoza kwenye kutangaza habari njema ya neema ya Mungu (Euangelion) pamoja na unabii duniani kote.Kwa pamoja ni waandishi bora wa vitabu kama Habari Njema, Intimacy, Prayer Banks, Supernatural power of the Believer n.k. Uebert na Bebe Angel ni wazungumzaji wanaotafutwa kwenye mikutano sehemu mbalimbali duniani, ni viongozi wa kidunia. Wanatambulika na kuheshimika kwa maono yao, uvumbuzi na ujasiri wao. Kama waanzilishi wa Kanisa la Good News (Spirit Embassy), na wenye ofisi ya kinabii, wamegusa maisha ya mamilioni ya watu ulimwenguni kupitia mapenzi yao ya kuvuna nafsi na kuleta ufunuo wa habari njema ya neema ya Mungu (Euangelion)..



**Mithali 4:23**
**Linda moyo wako kuliko yote uyalindayo; Maana ndiko zitokako chemchemi za uzima.**
**Ufahamu wako ni mlango wa kuingilia moyoni mwako. Kwa hivyo ikiwa unapaswa kulinda moyo wako, ni wapi bora zaidi kuanza kupalinda kuliko ufahamu wako? Hiyo inamaanisha unahitaji kuweka ulinzi kwenye akili yako, mawazo yako, na mchakato wako wa kufikiria. Kumbuka, Biblia inatuambia kwamba kama vile mtu afikirivyo moyoni mwake, ndivyo alivyo.**

Ondoa upotovu kinywani mwako; weka mazungumzo mabaya mbali na midomo yako. Ndivyo hasa ubaya unavyoingia moyoni mwako. Acha macho yako yatazame mbele, elekeza macho yako moja kwa moja mbele yako. Mungu anapokupa Neno Lake kuhusu maisha yako - kazi yako, familia, ndoa, watoto, fedha, au chochote kile - usipoteze mwongozo Wake. Usiseme vitu visivyo sahihi au nje ya kile Mungu amesema juu yako. Tamka Neno Lake na utazame mbele moja kwa moja. Kataa kuhamishwa kutoka kwenye Neno la Mungu linalohusu maisha yako, na utatoka na ushuhuda. Kumbuka moyo wako ni wajibu wako.

## UKIRI WA KINABII

**Niko vile Mungu anasema mimi niko. Ninacho kile Anachosema ninacho, na leo ninahama kutoka utukufu kwenda utukufu. Mimi ni mafanikio katika Kristo, na vitu vyote vinafanya kazi pamoja kwa faida yangu, kwa jina la Yesu!**

**SOMO LA ZIADA**
Warumi 12: 2



**2 Wakorintho 8: 9**
**Maana mmejua neema ya Bwana wetu Yesu Kristo, jinsi alivyokuwa maskini kwa ajili yenu, ingawa alikuwa tajiri, ili kwamba ninyi mpate kuwa matajiri kwa umaskini wake.**
**Baada ya kuzaliwa mara ya pili, umaskini haukubaliki kabisa maishani mwako. Ninajua kuna watu ambao wanaamini Wakristo wanapaswa kuwa maskini, lakini hiyo ni kwa sababu ya kukosa kwao kuelewa Maandiko. Umaskini sio ukosefu wa pesa au mahitaji mengine muhimu ya maisha. Kwa kweli ni kulemaa kwa uwezo wa akili wa mtu.**

Utajiri wote katika ulimwengu huu ni wako ikiwa umezaliwa mara ya pili. Mara tu utakapokubali kweli hii rohoni mwako na kuiruhusu itawale mawazo yako, itakupa mtazamo mpya. Haitawezekana kwako kutembea kwenye uhaba. Biblia inasema Yesu alikuwa maskini ili sisi, kwa umaskini wake, tuwe matajiri (2 Wakorintho 8: 9).

Hakuchukua juu yake dhambi za ulimwengu tu bali pia athari za dhambi, mojawapo ikiwa ni umasikini. Hii ndio sababu kila Mkristo lazima aukatae umasikini. Kwa hivyo, puuza na kukataa maisha ya chini; usiishi kama muhanga.

## UKIRI WA KINABII

**Mimi ni mrithi pamoja na Kristo, ulimwengu ni mali yangu, na hakuna kitu kizuri kilichozuiwa kwangu. Ninaishi katika kwenye maisha ya utele mwingi; maisha yangu ni uthibitisho wa upendo na neema ya Mungu. Haleluya!**

**SOMO LA ZIADA**
1 Wakorintho 3:21



**Waefeso 1: 3**
**Atukuzwe Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, aliyetubariki kwa baraka zote za rohoni, katika ulimwengu wa roho, ndani yake Kristo; Mungu tayari amekupa nafsi yake, Ufalme wake, na kila kitu! Unapoingia ndani ya Kristo, kila kitu ni chako. Hakuna kitu chochote zaidi cha Yeye kukupa kwa sababu wewe ni mrithi pamoja naye. Kwa hivyo, acha kuhangaika. Furahia maisha yako katika Kristo.**

Tunasoma katika mstari wetu wa ufunguzi kwamba tumebarikiwa na baraka zote za kiroho, na zote inamaanisha kila kitu ambacho unaweza kuhitaji. Hakuna kilichoachwa. Kumbuka, tayari amekubariki (usisahau ni katika wakati uliopita), sio baada ya kufunga na kuomba. Ni mpango uliokamilika. Acha kuhangaika na afya yako, matokeo yako, au fedha. Acha kuhangaika katika akili yako, na uchague maisha ya pumziko (Isaya 26: 3)."Kung'ang'ana" kwenye maombi ili Atimize ahadi zake ni juhudi katika ubatili. Ishi Neno na katika Roho. Utagundua kuwa kila kitu unachoweza kutaka kipo katika njia ambayo Yeye alikupa utembee. Jina lake lihimidiwe milele

## UKIRI WA KINABII

**Ninafanya kazi katika nuru ya Neno la Mungu. Nina ufahamu juu ya mahitaji tele ambayo Baba ameyatoa kwa ajili yangu, na ninayafurahia kikamilifu. Haleluya!**

**SOMO LA ZIADA**
2 Petro 1: 3



**Mathayo 6: 31-32**
**Msisumbuke, basi, mkisema, Tule nini? Au Tunywe nini? Au Tuvae nini? Kwa maana hayo yote Mataifa huyatafuta; kwa sababu Baba yenu wa mbinguni anajua ya kuwa mnahitaji hayo yote.**

Kwa nini mtu yeyote asome maneno haya ya Yesu na bado awe na wasiwasi juu ya chochote? Anajua yote unayohitaji ili uwe na maisha bora. Kwa hivyo, kataa kuwa na wasiwasi juu ya nguo mpya unayohitaji, au midoli mipya unavyotaka.Ikiwa utapata wasiwasi juu ya kitu chochote, inuka na sema kwa sauti, "Nakataa kuwa na wasiwasi!" Kisha, ingia kwenye Biblia yako na uanze kusoma na kutafakari Neno la Mungu. Unaona, tiba ya kuwa na wasiwasi ni kuishi katika Neno la Mungu. Biblia inasema, " Msijisumbue kwa neno lo lote; bali katika kila neno kwa kusali na kuomba, pamoja na kushukuru, haja zenu na zijulikane na Mungu."Angalia, ndugu na dada, inasema msijisumbue kwa neno lolote. Hiyo inamaanisha kuwa hakuna jambo maalum ambalo unaweza kuwa na wasiwasi nalo kwa sababu ni kubwa. Hapana mara elfu! Shikilia Nenona kukataa kuwa na wasiwasi!

## UKIRI WA KINABII

**Sina wasiwasi kwa kuwa moyo wangu umejengwa juu ya Neno. Nimemshinda Shetani, ulimwengu, na kila hali, kwa kuwa aliye Mkuu anaishi ndani yangu. Haleluya!**

**SOMO LA ZIADA**
Wafilipi 4: 6-7



**Marko 11:23**
**Amin, nawaambia, Ye yote atakayeuambia mlima huu, Ng'oka ukatupwe baharini, wala asione shaka moyoni mwake, ila aamini kwamba hayo asemayo yametukia, yatakuwa yake.**

Mungu anasema kwamba tutakuwa na chochote tunachokitamka. Kwa hivyo chochote tunachotaka kuwa nacho, tunaweza kukitamka kisha tukawa nacho. Kwa bahati mbaya, watu mara nyingi hutamka kile wasichotaka, kitu ambacho kinawaweka haswa mahali ambapo hawataki kuwa.Hata katika maombi, waumini wengi wako bize kumwambia Mungu jinsi shida zao zilivyo kubwa badala ya kugeukia milima yao na kuambia jinsi Mungu wao alivyo mkubwa. Mlima wowote wa shida ulionao, iwe mlima wa madeni au hali mbaya ya kiafya, mara tu unapochagua kutamka habari njema ya neema ya Mungu juu ya kila hali, tayari unajiweka mahali pa muujiza.Haijalishi kile kinachoonekana kuwa kimekufa na kuzikwa maishani mwako leo. Unapochagua kusema habari njema tu, unateka katika nguvu za Mungu, na kila mlima utahama.

## UKIRI WA KINABII

**Leo ninachagua kutamka uzima juu ya familia yangu, juu ya biashara yangu. Nguvu ya Mungu inasababisha vitu vyote kufanya kazi pamoja kwa faida yangu, katika Jina la Yesu!**

**SOMO LA ZIADA**
Warumi 10:10



**Isaya 58: 8**
**Ndipo nuru yako itakapopambazuka kama asubuhi, na afya yako itatokea mara; na haki yako itakutangulia; utukufu wa BWANA utakufuata nyuma ukulinde.**

Je! Unaishi maisha ya kujuta ukifikiria, "Laiti kama...?" Laiti ningekuwa na elimu ya chuo ... Laiti ningeoa mke sahihi... Laiti ningepata kazi nyingine... Laiti nisingefanya kosa hilo la kijinga...

Je! Maisha yako ya zamani yanakuibia furaha ya leo? Basi sahau zamani yako! Mungu amekusamehe dhambi zako zote. Amekusamehe kabisa na kutangaza, "Dhambi zao na uasi wao sitaukumbuka tena kabisa" Andiko letu la leo linasema utukufu wa BWANA utakufuata nyuma ukulinde. Popote uendapo, utukufu wake unafunika mambo yako ya zamani. Sio zamani tena ile unayoijua kwa sababu utukufu wake umeshuka juu yake. Zamani yako imepita. Imefutwa. Imekwenda! Kwa hivyo, usiruhusu maisha yako ya zamani yakunyang'anye furaha ya leo tena!

## UKIRI WA KINABII

**Mimi ni mtu mpya katika Kristo; mambo yote yamekuwa mapya. Sijui chochote dhidi yangu. Maisha yangu yamefichwa ndani ya Kristo, haleluya!**

**SOMO LA ZIADA**
2 Wakorintho 5:17; Waebrania 10:17



**Waebrania 11: 1**
**Basi imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo yasiyoonekana.**

Imani ni bayana. Sio wazo tu; ni uthibitisho. Tunapozungumza juu ya imani, ni kaka na dada wa kweli, na Bibilia inaiita uthibitisho.

Ikiwa nitapata visukuku vya dinosaria, visukuku sio dinosaria halisi. Hivyo ni ushahidi tu wa uwepo wao. Sasa nina uthibitisho kwamba jambo hili ni la kweli. Ndiyo sababu imani haiwezi kushindwa kamwe. Ni hati ya kumiliki hali halisi isiyoonekana. Unapotafakari na kusikiliza Neno la Mungu, ushahidi wa uponyaji wako unakujilia.Imani ni kifaa cha kiroho cha kufanya chochote kutokea kwa ajili yako. Una jukumu la kuyafanya maisha yako iwe jinsi unavyofikiria. Hali za maisha yako ambazo haukuziunda hazina uhalisia kwenye mafanikio yako na ushindi wako. Imani ni ushindi wetu kwa Jina la Yesu!

## UKIRI WA KINABII

**Imani yangu ni ushindi unaoshinda ulimwengu. Nilizaliwa, sio kwa mbegu inayoweza kuharibika, lakini kwa mbegu isiyoweza kuharibika na 'isiyoweza kuambukizwa' – ambayo ni Neno la Mungu ambalo huishi na kukaa milele.**

**SOMO LA ZIADA**
Warumi 12: 3



**1 Petro 1:23**
**Kwa kuwa mmezaliwa mara ya pili; si kwa mbegu iharibikayo, bali kwa ile isiyoharibika; kwa neno la Mungu lenye uzima, lidumulo hata milele..**

Unapolipokea Neno la Mungu, unapokea maisha ya chochote linachokizungumzia. Chochote unachosikia kutoka kwa Mungu ni mbegu ya kuzaa ndani yako, au kwako, kile inakizungumzia. Kwa mfano, tunapohubiri na kufundisha uponyaji wa kimungu, msikiaji hupokea mbegu ya uponyaji, inayozaa uponyaji na afya.
Vivyo hivyo, tunapofundisha Neno la Mungu juu ya mada ya fedha, hutoa mbegu ya baraka na miujiza ya kifedha. Hiyo ndiyo nguvu ya Neno la Mungu! Ukristo sio dini.Yesu Kristo alikuwa Neno la Mungu aliyefanyika mwili (Yohana 1:14). Sisi pia tulizaliwa mara ya pili kwa mbegu ile ile (Neno). Ndivyo tulivyosoma katika mstari wetu wa ufunguzi. Una maisha sawa na Mungu mwenyewe, kwa sababu umezaliwa na Neno — mbegu ya Mungu usioharibika.

## UKIRI WA KINABII

**Nimezaliwa na mbegu isiyoharibika ya Neno; kwa hivyo, maisha yangu yanadumishwa na Neno. Siwezi kamwe kushindwa katika maisha haya. Ninahama kutoka utukufu kwenda utukufu kwa Jina la Yesu!**

**SOMO LA ZIADA**
Yohana 1:14



**Waefeso 4: 7**
**Lakini kila mmoja wetu alipewa neema kwa kadiri ya kipimo cha kipawa chake Kristo.**

Sote tumepewa neema ya kukua kwenda juu maishani. Neno la Kiyunani lililotafsiriwa kama neema katika andiko letu la leo ni "charis," ambayo ni mzizi wa neno la Kiingereza "charisma." "Charis" inamaanisha ushawishi wa kimungu juu ya roho ya mwanadamu unaojidhihirisha nje kwenye maisha ya mwanadamu, kwa kuzaa upendeleo na kibali, uzuri, nia njema, kupendeka na uwezo.Ni utukufu wa Mungu katika roho yako, ambao unaakisi kwa nje. Neema hii husababisha upendeleo na utukufu kuzidi maishani mwako. Neema ya Mungu maishani mwako ni uwezo wa kiungu ndani yako kukufanikisha katika kila jambo. Na unapaswa kukua katika neema hiyo: "…kueni katika neema, na katika kumjua Bwana wetu na Mwokozi Yesu Kristo…." (2 Petro 3:18).

Neema ni nguvu ya kuinuliwa. Ni jambo linalosababisha maisha yako kuhama kutoka ngazi moja kwenda nyingine. Ndio maana Maandiko yanashauri kwamba ukue katika neema. Kila mtoto wa Mungu amepewa neema kwa utele (Warumi 5:17), lakini kiwango ambacho unairuhusu kiakisi ni juu yako. Kadiri unavyojaza moyo wako na Neno la Mungu na kumruhusu Roho Mtakatifu afanye kazi maishani mwako, ndivyo neema ya Mungu itakavyodhihirika maishani mwako kwa ukuu.

## UKIRI WA KINABII

**Bwana ameniweka kwenye maisha ya kiungu kwa neema yake. Kuinuliwa ni kwangu. Uwezo wangu ni wa Mungu, Haleluya!**

**SOMO LA ZIADA:** Warumi 5:17



**Mathayo 15:26 -27**
**Akajibu, akasema, Si vema kukitwaa chakula cha watoto na kuwatupia mbwa. Akasema, Ndiyo, Bwana, lakini hata mbwa hula makombo yaangukayo mezani pa bwana zao.**

Hili ni andiko mojawapo ambalo wengi hujaribu kulikwepa katika mahubiri yao. Yesu hakuwa na wasiwasi juu ya kuwa sahihi kisiasa kama wengi wetu leo. Alimwita mwanamke huyu waziwazi, ambaye alikuwa akimsihi amponye binti yake, mbwa. Lakini hiyo sio hata mada yangu hapa. Nataka uone kitu kingine.Angalia jibu la Bwana kwa mwanamke, " Si vema kukitwaa chakula cha watoto na kuwatupia mbwa." Subiri kidogo, Yesu anaita uponyaji chakula cha watoto. Kwa maneno mengine, namna ile ile ambayo mimi na wewe daima tunahakikisha kwamba tunawapatia watoto wetu chakula kila siku, ndivyo nguvu ya Mungu iko kila wakati kuponya. Kama vile mtoto wako alivyo na haki ya kuomba chakula anapokuwa na njaa, ndivyo tunavyoweza kuliitia jina la Bwana na kupokea uponyaji leo.Uponyaji ni wako leo. Baba yako tayari amekuapatia hitaji lako la kuwa mzima. Nakemea kila ugonjwa ambao unashambulia mwili wako kwa Jina la Yesu. Ninaamuru saratani hiyo iondoke kwa Jina kuu la Yesu!

## UKIRI WA KINABII

**Ninapokea uponyaji wangu kwa jina la Yesu. Ugonjwa hauna nafasi katika mwili wangu; Ninatembea katika afya ya Mungu tangu leo na kuendelea!**

**SOMO LA ZIADA**
1 Petro 2:24



**Waefeso 2: 6**
**Akatufufua pamoja naye, akatuketisha pamoja naye katika ulimwengu wa roho, katika Kristo Yesu;**
**Katika Ukristo, hatujaitwa kupigana na shetani. Shetani, Ibilisi, ni adui yetu, lakini tayari ameshindwa! Amehukumiwa, na sisi ndio tumepewa mamlaka ya kutekeleza hukumu yake!**

Kwa hivyo, hatupigani naye; tunatekeleza hukumu ambayo tayari imepitishwa kwake. Ni sehemu ya urithi wetu katika Kristo: "Kuwafanyia hukumu iliyoandikwa – hii ndiyo Heshima ya watauwa wake wote. Haleluya!" (Zaburi 149: 9).Katika Yohana 16:11, Yesu alisema, "mkuu wa ulimwengu huu amekwisha kuhukumiwa." Hiyo inamaanisha Shetani amehukumiwa. Haleluya! Una jukumu la kumuweka Shetani mahali anapostahili - chini ya miguu yako! Ndio maana biblia inasema kumtupa nje! Haupaswi kushindana na Shetani; mfukuze tu.

## UKIRI WA KINABII

**Hakuna silaha iliyoundwa dhidi yangu itakayofanikiwa. Hakuna mabaya yatakayonipata. Elfu wataanguka, na kumi elfu upande wangu wa kuume, lakini haitanikaribia, kwa Jina la Bwana Yesu.**

**SOMO LA ZIADA**
Zaburi 149: 9; Yohana 16:11



**1 Wathesalonike 5:18**
**shukuruni kwa kila jambo; maana hayo ni mapenzi ya Mungu kwenu katika Kristo Yesu.**

Shukrani inaachilia nguvu za Mungu kuanza kufanya kazi katika maisha yako. Angalia maandiko hayasemi mshukuru Mungu kwa kila kitu, lakini inasema "katika" kila kitu. Haijalishi maisha yanakutupia nini, unahitaji kuendelea kumshukuru Mungu, kwani kulia kunaweza kudumu usiku kucha, lakini furaha inakuja asubuhi.

Je! Haishangazi kwamba hata linapokuja suala la vitu tunavyohitaji katika maisha yetu, Mungu anataka sisi tumwendee na mtazamo wa shukrani kwa kile tunachoomba? Kamwe usimpe adui kuridhika kwa kufikiria amefanikiwa kuharibu siku yako. Ni kupitia shukrani ndiko mafanikio yako yapo.

## UKIRI WA KINABII

**Leo nimesimama nikiwa mshindi katika kila hali nitakayokabiliana nayo. Sifa zangu zina uwezo wa kuleta muujiza wangu. Sina wasiwasi!**

**SOMO LA ZIADA**
Waefeso 3:20



**Luka 15:20**
**Akaondoka, akaenda kwa babaye. Alipokuwa angali mbali, baba yake alimwona, akamwonea huruma, akaenda mbio akamwangukia shingoni, akambusu sana.**

Katika mfano wa mwana mpotevu (Luka 15: 11-24), baba hakusema hata neno moja juu ya hasara au upotevu, ingawa mtoto wake alikuwa amepoteza urithi wake kwa kuishi kwa hovyo. Baba aliona tu kurudi nyumbani kwa mtoto wake kama fursa ya kumwonyesha jinsi anavyompenda, na kumrudishia kile alichokuwa amepoteza.Kama baba katika mfano huu, ni hamu ya Baba yako wa mbinguni kukukumbatia na kukuonyesha jinsi unavyopendwa. Na ni fahali Yake kukurudishia kile ulichopoteza.Haijalishi umepoteza nini huko nyuma au ni makosa gani ambayo umefanya; Mungu anataka kukurudisha katika nafasi yako unayostahili. Hii ndio sababu anasema nitarudisha miaka iliyoliwa na nzige. Ana uwezo wa kuweka sawa mahusiano hayo yalioshindikana na kufufua biashara na afya yako inayodhorota. Habari Njema ni kwamba Mungu hayupo kukuadhibu kwa yaliyopita, lakini anataka kukumwagia baraka zake leo. Yaliyo bora bado yanaendelea kuja!

## UKIRI WA KINABII

**Mambo yangu ya kale hayawezi kunizuia kamwe. Ninabadilishwa kutoka utukufu kwenda utukufu. Ninarudisha kila kitu ambacho adui ameiba kwa Jina kuu la Yesu!**

**SOMO LA ZIADA**
Yoeli 2:25



**Warumi 5:20**
**Lakini sheria iliingia ili kosa lile liwe kubwa sana; na dhambi ilipozidi, neema ilikuwa nyingi zaidi;**
**Mtume Paulo alikuwa akihubiri neema ya Mungu kwa kiwango kikubwa sana kiasi kwamba alieleweka vibaya na kushtakiwa kwamba anawaambia watu watende dhambi zaidi ili neema ipate kuzidi. Kwa kweli, hiyo haikuwa hivyo.**

Paulo hakuwahi kusema, "Tufanye dhambi zaidi ili neema ipate kuzidi." (Na kwakweli, mimi sijawahi.) Dhambi ni mbaya, na husababisha matokeo mabaya. Lakini umeona katika maandiko ya leo ni nini haswa husababisha dhambi kuongezeka?

Soma andiko la leo tena. Paulo anasema waziwazi kwamba sheria iliingia ili dhambi ipate kuongezeka. Maana yake ni kwamba kadiri unavyohubiri sheria, ndivyo dhambi itakavyokuwa nyingi. Kwa maana nguvu ya dhambi ni sheria (1 Kor. 15:56). Kwa hivyo, unapoona dhambi na unahubiri zaidi sheria, unaongeza kuni kwenye moto! Shikilia Habari Njema, na neema itazidi!

## UKIRI WA KINABII

**Nimeokolewa kwa neema, na ninayaweza mambo yote kupitia Kristo. Dhambi haina tena nguvu juu yangu. Haleluya!**

**SOMO LA ZIADA**
Warumi 7: 8



**Warumi 5: 8**
**Bali Mungu aonyesha pendo lake yeye mwenyewe kwetu sisi, kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu, tulipokuwa tungali wenye dhambi.**

Niko hapa kukuambia bila uvuli wa shaka kwamba Mungu anakupenda na upendo wa milele. Upendo wake kwako hauna masharti (Tito 3: 3-5). Ni upendo ulio halisi sana, safi kabisa, na wa kushangaza. Hauna uhusiano wowote na utendaji wako, lakini una kila kitu cha kufanya na wewe ni nani machoni pake.Chagua kuamini sawa juu ya jinsi Mungu anavyokupenda leo. Inaleta tofauti zote ulimwenguni jinsi kwa haraka unavyoweza kurudi na kupiga magoti, na kutoka imani hadi imani na nguvu hadi nguvu katika kutembea kwako na Yeye.Unapendwa sana na Baba yetu wa mbinguni. Kwa kweli, Biblia inasema wakati tulikuwa bado wenye dhambi, Kristo alikufa kwa ajili ya wasiomcha Mungu.Si zaidi sasa kwa kuwa wewe ni kiumbe kipya ndani Yake? Hebu hii iweukiri wako na mtazamo wako. Wewe ni mwana wa pendo lake!

## UKIRI WA KINABII

**Mimi ni hazina ya kipekee kwa Mungu, nimezaliwa upya na maisha ya kiungu ya utukufu, ubora na nguvu katika roho yangu!**

**SOMO LA ZIADA**
Tito 3: 3-5



**2 Wakorintho 4:13**
**Lakini kwa kuwa tuna roho ile ile ya imani; kama ilivyoandikwa, Naliamini, na kwa sababu hiyo nalinena; sisi nasi twaamini, na kwa sababu hiyo twanena;**

Haitoshi kwa wewe tu kujua Neno katika moyo wako. Lazima uliseme. Hapo ndipo nguvu iliyofichika inakuwa nguvu halisi. Wakati Bwana wetu Yesu alipojaribiwa nyikani, hakufikiria tu juu ya maandiko. Aliyatamaka kwa sauti.

Unaweza kukariri maelfu ya maandiko, lakini ikiwa hutajifunza kusema, "Imeandikwa," na kuachilia Neno, hakutakuwa na nguvu. Nguvu za Mungu zipo, lakini zote zimelala tuli ndani yako. Unapotamka, ni kana kwamba Mungu anazungumza. Neno la Mungu kinywani mwako ni kama vile Mungu anatamka. Amina! Ndugu na dada kuamini Neno ni vizuri, lakini haitoshi. Ulipewa kinywa chako kuchora njia ya maisha yako kwa kutumia Neno la Mungu. Leo, tumia Neno kuleta katika usawa kitu chochote ambacho hakiendani na mpango wa Mungu kwa maisha yako.

## UKIRI WA KINABII

**Vitu vyote vinafanya kazi pamoja kwa faida yangu. Kuna kuinuliwa katika fedha zangu, kazi, biashara, familia na kila kitu kinachonihusu, katika Jina la Yesu!**

**SOMO LA ZIADA**
Waefeso 6:17



**Mwanzo 13: 2**
**Naye Abramu alikuwa ni tajiri sana kwa mifugo, kwa fedha, na kwa dhahabu**

Ninafurahi sana kwamba Mungu alielezea utajiri wa Ibrahimu kwa ubayana. Mungu lazima aliona mbele kizazi cha watu ambao watasema kwamba Yeye yuko kinyume cha watu wake wanaopata mafanikio ya kifedha. Kwa hivyo alisema wazi katika Neno Lake kwamba Ibrahimu alikuwa tajiri sana katika mifugo, fedha, na dhahabu. Abraham hakuwa tajiri tu kiroho.Ndugu na dada, Mungu hashindani wewe kuwa na mali, lakini hakika yeye ni dhidi ya utajiri kukutawala wewe. Mara zote Bwana hukupa pesa, jukumu maalumu na mafanikio kwa kusudi maalumu.Anakubariki, na unapobarikiwa, unanaweza kuwa chombo cha kuwabariki wengine.
Usipende pesa na kuwatumia watu. Tumia pesa kuwapenda watu. Na ikae moyoni mwako mara moja na kwa daima kwamba ni hamu ya Mungu kukuona ukifanikiwa kifedha na kuwa na zaidi ya kutosha kubariki wengine!

## UKIRI WA KINABII

**Nimejaa baraka za ki-Mungu. Baraka hizi zinanifanya nistawi katika yote ninayofanya. Nimekuwa kama mti uliopandwa kando ya mto wa maji.**

**SOMO LA ZIADA**
Mithali 10:22



**2 Mambo ya Nyakati 20:15**
**....... Msiogope, wala msifadhaike kwa ajili ya jeshi kubwa hili; kwani vita si yenu bali ni ya Mungu.**

Adui alipokuwa amekuja dhidi ya Yuda, walimlilia Mungu kwa kukata tamaa sana. Ilionekana kana kwamba wote walikuwa wameshindwa hata kabla hawajaenda vitani. Walizidiwa idadi na maadui zao, na hali zote zilikuwa zilikuwa kinyume chao. Yote yalionekana kutokuwa na tumaini.Lakini ndipo Mungu anageuka na kusema, vita sio yenu bali ni Yangu. Hautahitaji kupigana. Adui alikuwa amefanya mahesabu na kuleta askari wote wa miguu na wapanda farasi aliohitaji ili kumshinda Yuda. Lakini kile ambacho hakuwa amejua ni kwamba Yehova mwenyewe alikuwa akielekea kwenda vitani.Haijalishi uchumi wako unaonekana mbaya kiasi gani leo au ripoti ya daktari inasema nini juu ya afya yako.Bwana Mungu mwenyewe anakuja kupigania kwa niaba yako, yote yamekwisha pangwa, na unashinda. Hii ndiyo sababu Bibilia inasema, "Yeye hutufanya siku zote tushinde katika Kristo." Ndio maana biblia inaiita vita nzuri ya imani. Ni vita nzuri kwa sababu unashinda. Anaweza kugeuza kipato chako, kuponya mwili wako, kurudisha ndoa yako. Umeunganishwa na muujiza wako hivi sasa. Upokee kwa Jina la Yesu.

## UKIRI WA KINABII

**Bwana ni msaada wa karibu sana wakati wa uhitaji na hunifanya mshindi katika kila hali.**

**SOMO LA ZIADA**
Yoshua 1: 5



**Yohana 1:14**
**Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu; nasi tukauona utukufu wake, utukufu kama wa Mwana pekee atokaye kwa Baba; amejaa neema na kweli.**

Wakati Bwana Yesu alikuwa akitembea hapa duniani, Alikuwa udhihirisho na maelezo kamili wa upendo wa Mungu kwa uumbaji wake. Andiko letu la leo linasema kwamba alikuwa amejaa neema na kweli. Sasa, ingawa Bwana hatembei tena kati yetu katika mwili, nina habari njema kwako.Neno hilo hilo lililokuwa mwili katika siku za huduma yake hapa duniani halijapoteza hata chembe moja ya nguvu na neema. Bado unaweza kuiishi nafsi ya Bwana Yesu na kumuelezea kupitia neno Lake. Ikiwa unahisi ulimwengu wote uko dhidi yako hivi sasa, Neno Lake linasema kwamba Yeye hatakuacha kamwe wala kukutelekeza. Je, ni mgonjwa katika mwili wako leo? Neno lake linatangaza kwamba "kwa kupigwa kwake, mliponywa."

Haijalishi unahitaji nini leo, neema yake inatosha kwako. Unapoangalia katika Neno la Mungu leo, neema inaachiliwa juu yako kuvunja kila mazoea mabaya, kuponya kila moyo uliovunjika kwa jina la Yesu!

## UKIRI WA KINABII

**Neema ya Mungu inanitosha. Ninayaweza mambo yote kupitia Kristo anitiaye nguvu! Aliye ndani yangu ni Mkuu kuliko yeye aliye ulimwenguni. Haleluya!**

**SOMO LA ZIADA**
Warumi 8: 3-4



**Waefeso 5: 18-19**
**Tena msilewe kwa mvinyo, ambamo mna ufisadi; bali mjazwe Roho; mkisemezana kwa zaburi na tenzi na nyimbo za rohoni, huku mkiimba na kumshangilia Bwana mioyoni mwenu;**

Mungu ametoa nguvu kubwa sana kwa muumini. Una nguvu ya kusababisha mabadiliko na kuleta suluhisho kwa ulimwengu huu. Kwa kweli, wewe ni nuru katika ulimwengu huu wa giza na ulioharibika. Nuru yako inapaswa kuangaza kuondoa giza na kuzileta Mbingu Duniani. Lakini lazima ujazwe na Roho ili uweze kufanikisha hili. Njia mojawapo ya hakika ya kujazwa ni kwa wewe kujisemesha mwenyewe katika zaburi na tenzi, huku ukimwimbia Bwana. Utataharakishwa katika roho yako na kujichaji tena. Je! Unajihisi mnyonge na umevunjika moyo leo? Vyema, unaweza kufanya kitu juu ya hili. Hauhitaji hata mtu mwingine yeyote. Unaweza kujisemesha mwenyewe katika zaburi na tenzi. Unaweza kujichochea rohoni kwa kuomba kwa kunena kwa lugha na kuimba nyimbo moyoni mwako kwa Bwana. Unapofanya hivi, masononeko hayatakuwa na chaguo zaidi ya kukuacha. Maumivu ya kichwa hicho yatapaswa kuondoka kwa Jina la Yesu!

## UKIRI WA KINABII

**Ninayaweza mambo yote kupitia Kristo anitiaye nguvu. Nimetiwa nguvu maradufu na Roho Mtakatifu ili kushinda leo kwa Jina la Yesu!**

**SOMO LA ZIADA**
Matendo 6: 8



**Warumi 6:13**
**bwala msiendelee kuvitoa viungo vyenu kuwa silaha za dhuluma kwa dhambi; bali jitoeni wenyewe kwa Mungu kama walio hai baada ya kufa, na viungo vyenu kwa Mungu kuwa silaha za haki.**

Mlipokuwa wadhambi, kutenda dhambi ilikuwa rahisi na karibu jambo la bila hata kufikiria. Kila kitu kukuhusu kilikuwa chini ya dhambi. Sasa kwa kuwa umeokoka na umekuwa mtoto wa Mungu, unaweza kutoa vivyo hivyo viungo vyako vyote kwa ajili haki. Sisi sasa ni watumwa wa haki. Unaona, kumuishia Mungu ni changamoto lakini sio kitu kigumu. Tunachohitaji kufanya ni kujisalimisha kwenye neema Yake na kuruhusu utambulisho wake ndani Yake utiririke kwa nje.Tunapojitoa ili kuwa kwenye nguvu na kani ya haki, tutajikuta tukifanya mambo yanayompendeza Mungu. Fikiria hadithi za Biblia za wanaume ambao walijiliwa na Roho juu yao, wanaume kama Samsoni. Walifanya mambo ya ajabu yaliyopita kawaida za wanadamu kwa sababu viungo vyao vilikuwa chini ya ushawishi wa Roho. Vivyo hivyo tutafanya ya ushujaa tutakapokubali haki na kuruhusu asili hiyo mpya ituongoze. Matokeo ya mwisho ni uzima.

## UKIRI WA KINABII

**Mimi sasa ni mtoto wa Mungu. Kilichokuwa kikiiwezesha dhambi maishani mwangu sasa kimekufa. Mimi sasa ni mtumishi na mtumwa wa haki. Akili yangu, ulimi wangu, na yote niliyo yako chini ya ushawishi wa neema. Bila kung'ang'ana, ninadhihirisha maisha ya  namna ya ki-Mungu. Asante, Baba!**

**SOMO LA ZIADA**
Warumi 6: 12-22; Waamuzi 14: 5-6



**Waebrania 13: 6**
**Hata twathubutu kusema, Bwana ndiye anisaidiaye, sitaogopa; Mwanadamu atanitenda nini?**

Unapopitia kipindi kigumu zaidi cha maisha yako, msaada, upendo na kujali kwa familia yako na marafiki zako huenda kukakosekana.Kuna Mmoja ambaye unaweza kuwa na hakika kila wakati kwamba unapoenda kwake, Yeye hatakunyima msaada Wake kamwe.

Upendo wake ni mkuu na wa kina zaidi kuliko bahari. Moyo wake uko tayari kila wakati kukukaribisha, na sikio lake huwa makini kila wakati kusikiliza sala zako zote. Huyu si mwingine ila ni Roho Mtakatifu, Mfariji na Mwandani wetu. Fanya uamuzi leo kumwamini Yeye katika kila jambo linalohusu maisha yako. Yuko karibu nawe kuliko nguo ambazo umevaa hivi sasa. Hatakuacha, wala kukutelekeza kamwe.

## UKIRI WA KINABII

**Nimepata ndani ya Yesu Kristo Rafiki mwaminifu. Ninajiweka kwake, na maisha yangu hayatakuwa sawa tena.**

**SOMO LA ZIADA**
Warumi 4:21



HabariNjema
KILA SIKU



**Hosea 4: 6**
**Watu wangu wanaangamizwa kwa kukosa maarifa…**

Shida yako kubwa hivi sasa kama mwamini sio kwamba unahitaji kufunguliwa lakini ni kwamba unakosa maarifa, sio upako, sio nguvu lakini maarifa! Ibilisi sio shida yako. Anajua tu jinsi ya kuutumia ujinga wako.Kuingia kwa Neno la Mungu huleta nuru. Kamwe huwezi kukosa msaada wakati unajua habari njema za Neno Lake. Una Mpanga mikakati wa Ajabu kwenye kona yako.

Paulo alisema sisi sio wajinga wa hila za adui. Leo, jivike silaha za Habari Njema ya Neno la Mungu. Fedha zako hazitakuwa na chaguo lingine isipokuwa kuanguka kwenye mstari wako. Dhoruba katika ndoa yako italazimika kukoma wakati unapoanza kutembea katika hekima ya Mungu. Amua kutokuishi mjinga wa ahadi na Habari Njema ya Mungu maishani mwako leo.

## UKIRI WA KINABII

**Sitakuwa mjinga juu ya ahadi za Mungu kwenye maisha yangu. Ninapoendelea kusikia Habari Njema ya neema yake, ninabadilishwa kutoka utukufu kwenda utukufu.**

**SOMO LA ZIADA**
Mithali 4: 7



**Warumi 4:17**
**(kama ilivyoandikwa, Nimekuweka kuwa baba wa mataifa mengi); mbele zake yeye aliyemwamini, yaani Mungu, mwenye kuwahuisha wafu, ayatajaye yale yasiyokuwako kana kwamba yamekuwako.**

Yesu alipomuona Simoni kwa mara ya kwanza, ambaye jina lake kwa Kiyunani linamaanisha "tete," alimbadilisha jina lake kuwa "Peter," ambalo linamaanisha "mwamba." Lakini je! Peter papo hapo alikua mtu mwenye tabia ya mwamba, imara, thabiti na isiyotikisika? Hapana, kwa muda mrefu, aliendelea kutenda kama tete unaoinamia kila uelekeo ambao upepo unavuma.

Mungu hakutuambia tuviite vitu hivyo ambavyo vipo kama vile vipo. Je! Ni nini maana ya kusema hilo kwa udhahiri? Maana Haitabadilisha chochote. Hapana, Mungu anatuambia tuviite vitu ambavyo havipo kana kwamba vimekuwapo, na vitakuwa hivyo!Ikiwa wewe ni mgonjwa katika mwili wako leo, anza kuita afya unayohitaji. Ikiwa ni kuinuliwa unakokuhitaji, fungua kinywa chako na uamuru kibali cha Bwana. Vitu vyote ni vyako. Haleluya!

## UKIRI WA KINABII

**Maneno yangu si ya kawaida; yamejazwa na nguvu ya kiungu, yakizalisha kile ninachoyatuma kukamilisha. Haleluya!**

**SOMO LA ZIADA**
Mithali 18:21



**Mathayo 6:33**
**Bali utafuteni kwanza ufalme wake, na haki yake; na hayo yote mtazidishiwa.**

Kwa sababu ni rahisi sana kutamani pesa na vitu ambavyo inaweza kukuletea, Bwana alianzisha mfumo ambao mafanikio ni matokeo ya kumtanguliza Mungu kwanza. Andiko letu la leo linasema, "Bali utafuteni kwanza ufalme wa Mungu na haki yake, na hayo yote mtazidishiwa."

Sababu ya kutokuweka hazina hapa duniani ni ili kwamba tusiivute mioyo yetu mbali na mambo ya Mungu. Ufunguo wa kufanikiwa katika Ufalme wa Mungu ni umoja wa kusudi.Huna uwezo wa kufanya mambo kwa ubora katika maeneo mawili kwa wakati mmoja. Ikiwa utamweka tu Mungu na Ufalme wake mbele katika kila eneo la maisha yako, atakuongezea utajiri wote unaohitaji. Je! Ni nini cha maana zaidi au muhimu kuliko kumjua Yeye? Tanguliza mambo ya kwanza kwanza.

## UKIRI WA KINABII

**Ustawi ni wangu kwa Jina la Yesu. Siwezi kushindwa. Nina maisha ya Mungu ndani yangu. Ninavuta kibali na fursa kila siku, kwa Jina la Yesu!**

**SOMO LA ZIADA**
Mithali 10:22



**Marko 5:34**
**Akamwambia, Binti, imani yako imekuponya, enenda zako kwa amani, uwe mzima, usiwe na msiba wako tena**

Ni mara ngapi umesikia ikisemwa kwamba imani humsogeza Mungu? Waumini wengi wamezoea dhana hii kwamba hutumia wakati wao kujaribu kumfanya Mungu afanye kitu fulani. Kwa kweli, hii inapingana na imani.Tambua kwamba alilofanya ili kuponywa yule mwanamke aliyekuwa anatokwa na damu ilikuwa ni kumgusa Yesu. Bwana hakuwahi kumwombea. Kwa hivyo muujiza huu uliwezekanaje? Ni kwa sababu Mungu alikuwa amekwisha kumpatia uponyaji. Kile alichopaswa kufanya ni kutumia imani yake na kunyakua kile ambacho ni haki yake. Kwa hivyo unahitaji nini katika maisha yako sasa hivi? Nina habari njema kwako. Mungu tayari amekifanya. Kiko tayari na kinakusubiri ukifikie kwa imani na kukinyakua!Unaona imani haimsogezi Mungu. Yeye siye ndiye aliyekwama; ni sisi. Imani pia haimfanyi Mungu kufanya chochote. Inatuhamishia sisi tu kwenye kile Mungu alichotutendea pale Kalvari miaka 2000 iliyopita. Yote tunayohitaji kuishi maisha yenye maana yalitolewa na Yesu kupitia ushindi wake dhidi ya msalaba na kaburi. Sasa wewe kama mtu binafsi unaweza kupata muujiza wako kwa kuwa na imani yako na kuifanyia mazoezi. Unaweza kuamini, na kupokea, ya ajabu!

## UKIRI WA KINABII

**Namtumikia Mungu mwenye nguvu ambaye kwake hakuna linaloshindikana. Hakuna jambo gumu au tatizo ambalo hajawahi kushinda. Ninajiweka sawa na ushindi Wake na kutangaza ushindi katika kila vita, kwa Jina la Yesu!**

**SOMO LA ZIADA:** Marko 11:24



**Isaya 55:11**
**ndivyo litakavyokuwa neno langu, litokalo katika kinywa changu; halitanirudia bure, bali litatimiza mapenzi yangu, nalo litafanikiwa katika mambo yale niliyolituma.**

Andiko la leo linafunua siri ya kufurahisha ya jinsi ya kulifanya Neno kufanya kazi. Mstari huo unasema Neno halitarudi kwa Mungu bure. Kwa hivyo Neno huwa na ufanisi katika safari yake ya kurudi. Chochote Mungu anazungumza juu yako, wewe kitamke. Mungu akisema utakuwa tajiri, unasema, "mimi ni tajiri!" Anaposema wewe ni mkuu kuliko maadui zako, unasema, "Mimi ni mkuu kuliko maadui zangu." Kwa kupigwa kwake uliponywa. Unapiga kelele, "nimepona!" Usisubiri chochote leo. Fanya Neno lifanye kazi kwa kulinena.Unahitaji nini leo? Ingia ndani ya Neno na anza kulithibitisha Neno hilo. Na unapolirudisha, nguvu hiyo ya kusababisha mabadiliko huachiliwa katika hali yako. Haleluya!

## UKIRI WA KINABII

**Neno linafanya kazi. Mimi ni kile Mungu anasema mimi niko. Mimi ni wa kifalme; hakuna kinachonifadhaisha! Nina nguvu ya kutengeneza utajiri na kukuza mawazo yangu kuwa vitu vyenye faida. Kwa kupigwa kwake niliponywa. Ninaamuru kwamba nina nguvu juu ya maadui zangu; hakuna kitakachozuia kupanuka kwangu kwa Jina la Yesu!**

**SOMO LA ZIADA**
Zaburi 107: 19-21



**Matendo 12: 7**
**Mara malaika wa Bwana akasimama karibu naye, nuru ikamulika mle chumbani, akampiga Petro ubavuni, akamwamsha, akisema, Ondoka upesi. Minyororo yake ikamwanguka mikononi.**

Marais wanalindwa na wafanyikazi wa usalama na wenye ujuzi na waliobobea zaidi katika nchi zao. Kwa sababu ya huduma ya siri za usalama, marais na watu wengine wanaoheshimiwa sana katika jamii wanaweza kutembea kwa uhuru na kufanya shughuli zao katika sehemu nyingi bila woga. Wewe pia una timu maalum, yenye zana nyingi ya mawakala wa siri wanaoitwa malaika. Ingawa hawaonekani kwa macho ya asili, malaika ni halisi na wanaathiri vitu katika ulimwengu wa mwili. Na kilicho bora ni kwamba Mungu ameahidi kukuagizia boma la malaika kwa ajili yako. Kama Mkristo, umefika kwenye Mlima Sayuni, ambapo kuna kundi kubwa la malaika. Katika andiko letu la leo, malaika alipofika, minyororo ya mwilini ilianguka kutoka kwa Petro, na akatoroka gerezani. Sasa fikiria una malaika zaidi ya mmoja upande wako. Hakika hakuna kinachoweza kukufunga. Hakika mambo yako yataenda tu. Unapoendelea na biashara yako leo, kuna malaika wamewekwa kimkakati ili kukusaidia. Kuna malaika anayeshughulikia kesi yako mahakani, kwa hivyo unashinda. Malaika ametumwa kuhakikisha barua yako ya maombi inafanikiwa. Sehemu yoyote ambayo unaweza kuwa,kutakuwa na uingiliaji kati wa malaika kuletea habari njema.

## UKIRI WA KINABII

**Ninatuma malaika kushinikiza kinyume cha shambulio lolote la mapepo. Kila kitu na kila mahali nitakokwenda leo tayari kumetayarishwa kwa ushindi wangu. Malaika wananilinda, na maisha yangu ni salama. Ninaingia katika hatua mpya na za kufurahisha za maisha yangu. Asante, Yesu!**

**SOMO LA ZIADA:** Matendo 12: 1-10



**Mwanzo 26:22**
**Akaondoka huko akachimba kisima kingine, wala hicho hawakukigombania. Akakiita jina lake Rehobothi, akasema, Kwa kuwa sasa BWANA ametufanyia nafasi, nasi tutazidi katika nchi.**

Mara nyingine, wakati mambo hayafanyi kazi, ni ishara kuwa uko mahali pasipo sahihi. Sio kila wakati ni jambo hili kwa sababu kuna vizuizi ambavyo vinahitaji tu juhudi zako za pamoja ili viondoke. Lakini unapokuwa ukijaribu na mambo hayaendi, inaweza kuwa wakati wa kubadilisha eneo. Isaka aliepuka magonvi na Wafilisti wakati walipopigania visima ambavyo alichimba na vilikuwa vyake kihaki kabisa. Walipogombania umiliki wa visima, kirahisi kabisa alihamia eneo lingine. Lazima uwe mwangalifu usipoteze nguvu zako, wakati, na rasilimali zako katika magomvi ya kiroho na ya kimwili ambayo hayazai matunda yoyote kwako. Ingia Rohoni na ujue ni wakati gani wa kufungua ukurasa mpya.Unapoendelea na biashara yako leo, naomba Bwana alinde na kuongoza hatua zako kwa Jina la Yesu. Akuweke mahali sahihi kwa wakati unaofaa kwa muujiza wako. Unashinda leo!

## UKIRI WA KINABII

**Bwana, nifunulie sehemu inayofuata uliyoitenga kwa ajili ya maendeleo yangu kuwapo. Ninakataa kuwa mahali ambapo ukuaji wangu umezuiliwa. Niko tayari kwa mabadiliko; Niko tayari na kukumbatia kiwango changu kijacho maishani. Ninakushukuru mapema kwa kuniongoza kwenye eneo langu linalozaa kwa wakati unaofaa. Amina!**

**SOMO LA ZIADA:** Mwanzo 26: 16-33; Ruthu 1:22, 4:13



**2 Wakorintho 3:18**
**Lakini sisi sote, kwa uso usiotiwa utaji, tukiurudisha utukufu wa Bwana, kama vile katika kioo, tunabadilishwa tufanane na mfano uo huo, toka utukufu hata utukufu, kama vile kwa utukufu utokao kwa Bwana, aliye Roho.**

Unapojifunza kuendesha gari, wakufunzi wanakuhimiza uelekee macho yako huko unakoenda, haswa wakati kuna trafiki inayokuja. Wanakuambia kwamba ikiwa utatazama macho yako kwenye magari yanayokuja, utajikuta unaendesha kuelekea kwao, na kusababisha ajali. Vivyo hivyo inaweza kusemwa juu ya maisha. Mlengo wako huamua mwelekeo wako.Mungu ametupa Neno lake ili lituelekeze na kutuongoza katika njia za kupendeza na amani. Unapozingatia kwenye Neno, unakuwa kile linazungumza juu yako. Unaanza kutumia mamlaka dhidi ya kila hali. Unaleta athari katika nyanja tofauti za maisha. Angalia tena maandiko. Yanasema tunaona utukufu na tunabadilishwa kuwa utukufu huo huo! Wewe halisi ni kile unachokiona kwenye kioo (Neno la Mungu). Na ikiwa Biblia inasema unaangalia utukufu kwenye kioo, kisha unakuwa utukufu wa Mungu. Haukukusudiwa kushindwa au kushushwa thamani. Haijalishi uko wapi hapa duniani, una asili kutoshindwa. Elekeza macho yako kwenye Neno Lake na utazame maisha yako yakibadilika mbele ya macho yako.

## UKIRI WA KINABII

**Macho yangu yako kwenye Neno. Ninakataa kuvurugwa na umbea na habari zingine mbaya. Hofu za watu wengine hazitalisha mlengo wangu. Nimewekwa kwenye njia lazima nifuate kwa Jina la Yesu!**

**SOMO LA ZIADA:** Waebrania 12: 1-2



**Mathayo 4: 4**
**Naye akajibu akasema, Imeandikwa, Mtu hataishi kwa mkate tu, ila kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu.**

Kama mtoto wa Mungu, wewe sio mtu asiye na msaada au wa kuwa kwenye matatizo katika kila hali inayokujia maishani. Kwa kweli, Neno la Mungu linakupa uwezo wa kudhibiti mambo ya ulimwengu huu. Mtume Paulo alisema Neno la Mungu lina kasi na nguvu, lina makali kuliko upanga wowote wenye makali kuwili. Hii ndio logos ya Mungu.Hii ndiyo sababu, kama Mkristo, unahitaji kukaa katika Neno. Lakini leo, nataka kuonyesha kitu ambacho kitafanya kazi hata haraka kuliko Neno la Mungu lililoandikwa, na hiyo ni rhema ya Mungu. Unaona, unapotafakari juu ya Neno la Mungu, na Neno hilo likajichimbia rohoni mwako, wakati hali zinapotokea, Roho wa Mungu anaweza kutumia Neno hilo ambalo liko rohoni mwako kukuandaa kwa rhema ya Mungu.Hii ndiyo sababu andiko letu la leo linasema kwamba mtu hapaswi kuishi kwa mkate tu bali kwa rhema ya Mungu. Ni neno maalum, kwa hali maalum, kwa mtu maalum. Pokea rhema yako kwa ajili ya leo! Unafanikiwa leo kwa Jina la Yesu! Kibali ni chako! Hakuna magonjwa yatakayoweza kujishikiza kwenye mwili wako! Hii ni siku yako. Nenda nje na ushinde!

## UKIRI WA KINABII

**Mimi ni zaidi ya mshindi. Rhema ya Mungu inafanya kazi ndani yangu. Hakuna silaha iliyoundwa dhidi yangu itakayofanikiwa, kwani Yeye aliye ndani yangu ni mkuu kuliko yeye aliye ulimwenguni. Leo ni siku yangu, haleluya!**

**SOMO LA ZIADA:** Luka 4: 9-12


UEBERTANGEL
MinisterialAssociation
UAMA IS AN EXCLUSIVE MEMBERSHIP PROGRAM BY PROPHET UEBERT ANGEL FOR PEOPLE FROM ALL WALKS OF LIFE WHO HAVE ONE THING IN COMMON – A DESIRE TO GROW IN MINISTRY
TO JOIN UAMA VISIT
WWW.UAMA.CO




WWW.BEVERLYANGEL.ORG



**Wafilipi 3: 13-14**
**Ndugu, sijidhanii nafsi yangu kwamba nimekwisha kushika; ila natenda neno moja tu; nikiyasahau yaliyo nyuma, nikiyachuchumilia yaliyo mbele; nakaza mwendo, niifikilie mede ya thawabu ya mwito mkuu wa Mungu katika Kristo Yesu.**

Ni rahisi kufikiria haupigi hatua yoyote unapozingatia kwenye kile usicho nacho au kile ambacho haukufanikiwa. Hofu itakufanya uzingatie kile unachofikiria ni kushindwa, lakini haitakupa muujiza wako. Hofu haina asili yake kwa Mungu, lakini imani ina asili kwa Mungu, na imani ndio tiba ya hofu. Imani iliyopunguzwa kuwa sehemu yake ya msingi ni mabishano na shetani. Ibilisi anasema hivi, na wewe unasema vile. Shetani anaposema kitu kinachokufanya uogope, sema, "Nina shaka."Una imani sawa na ile ya Mungu. Fikiria juu ya hilo. Imani ile ile ambayo Mungu alitumia kutamka ulimwengu uwepo ndiyo imani ile ile aliyoiweka katika roho yako. Sahau juu ya kile ambacho hakikuenda sawa na uelewe kuwa vitu vyote vinafanya kazi pamoja kwa faida yako. Unachofikiria kuwa ni kizuizi ni mpango wa mafanikio yako. Kamwe usielekeze macho yako kwenye kutofaulu. Angalia kwa macho ya imani kwenye kesho unayotaka kuwa nayo na anza kusema mafanikio yako na maendeleo yako kuwa hai. Unashinda hata iweje!

## UKIRI WA KINABII

**Ninaongozwa na Roho wa Mungu, na Yeye hunisababisha kushinda kila wakati. Mafanikio yangu hayapingiki. Maendeleo yangu hayaepukiki. Na maisha yangu ni mbele na juu tu!**

**SOMO LA ZIADA**
Warumi 12: 3; 8:28



**Wagalatia 2:20**
**Nimesulibiwa pamoja na Kristo; lakini ni hai; wala si mimi tena, bali Kristo yu hai ndani yangu; na uhai nilio nao sasa katika mwili, ninao katika imani ya Mwana wa Mungu, ambaye alinipenda, akajitoa nafsi yake kwa ajili yangu.**

Sijawahi kusikia mtu aliyekufa akilalamika juu ya bili anazopaswa kulipa, shida katika ndoa yake, au ripoti mbaya aliyoipata kutoka kwa daktari. Kwa maneno mengine, hayuko tena chini ya shida za maisha haya. Andiko letu la leo linatupa ufunuo wa kibinafsi wa Paulo. Anasema, "Nimesulubiwa katika Kristo." Ufunuo huo sio wa Mtume Paulo tu. Pia ni ukweli wako.Umesulubiwa pamoja na Kristo. Je! Unawezaje kuwa chini ya vitu vile vile watu ambao hawakusulubiwa wanakabiliwa? Ukweli ni kwamba wewe hauko chini ya hasara. Umesulubiwa kwa umasikini, magonjwa, kifo cha mapema, na kutofaulu. Ah, utukufu kwa Mungu! Wakati shetani anapojaribu kunong'oneza dalili za ugonjwa masikioni mwako, au anapojaribu kukushawishi kwamba hautaweza, shika mabega yako, simama kwa miguu na kusema, "Ibilisi, nimekufa kwa hayo!"

## UKIRI WA KINABII

**Mimi ni mrithi pamoja na Yesu Kristo. Utajiri wake ni utajiri wangu. Afya yake ni afya yangu. Ushindi wake ni ushindi wangu. Kila kitu ambacho ni chake ni mali yangu. Haleluya!**

**SOMO LA ZIADA**
Warumi 8: 16-17



**Wakolosai 1: 9**
**Kwa sababu hiyo sisi nasi, tangu siku ile tuliposikia, hatuachi kufanya maombi na dua kwa ajili yenu, ili mjazwe maarifa ya mapenzi yake katika hekima yote na ufahamu wa rohoni;**

Katika kifungu hapo juu, ningependa uone neno la pekee "maarifa." Neno hili katika tafsiri ya Kiyunani ni "epignosis," na linamaanisha maarifa kamili, mbali kabisa na mawazo au dhana. Haya ni maarifa halisi, sahihi, dhahiri au kamili.Kama vile Mtume Paulo, hamu yangu kwako sio tu kuwa na wazo au kufahamu kwa juu juu tu mapenzi ya Mungu. Badala yake, nataka ujue kabisa mapenzi yake kwenye maisha yako, kwani ndio ushindi wako!

Filemoni 1: 6 inasema mawasiliano ya imani yako yanakuwa na ufanisi kwa "epignosis" ya kila kitu kizuri, ambacho kiko ndani yako katika Kristo Yesu. Hiyo inamaanisha kuwa unapoletwa katika maarifa kamili na maalum ya mambo mema yote yaliyo ndani yako katika Kristo Yesu, udhihirisho wa imani yako unakuwa na tija zaidi. Utukufu kwa Mungu!

## UKIRI WA KINABII

**Roho yangu imeangaziwa kujua na kushika yote ambayo Mungu amenipa katika Kristo! Natembea katika uhalisi wa urithi wangu; Natembea katika maarifa kamili ya Kristo. Ninatembea katika ushindi, utawala, na mafanikio kila wakati, katika Jina la Yesu. Amina.**

**SOMO LA ZIADA**
Filemoni 1: 6



**Warumi 12: 2**
**Wala msiifuatishe namna ya dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza, na ukamilifu.**

Maandiko yanatuelekeza tusifuatishe ulimwengu huu, kwa sababu Mungu hataki tufikirie au tufanye kama wa ulimwengu. Kama Wakristo, tunapaswa kuwa tofauti. Maagizo ya pili ni kugeuzwa. Hii inamaanisha metamofosisi, kubadilishwa kuwa muundo au umbo jipya! Mabadiliko haya yanaweza kupatikana tu kwa kufanywa upya kwa nia ya mtu.Hii inamaanisha kubadilisha namna yako ya kufikiri kupitia Neno la Mungu. Maadili yako, maoni yako, mawazo yako na uchaguzi wako lazima utawaliwe na Neno la Mungu! Sisi ni wa ufalme tofauti, huo ni Ufalme wa Mungu, na maisha ambayo ametupatia kuishi ni tofauti na yale yanayojulikana na ulimwengu wote. Tunaishi katika afya na ustawi wa kimungu! Tunaishi maisha ya ushindi, yaliyojaa kusudi, na maisha haya tunayoishi yamejaa nuru na yamejaa utukufu. Tunachagua kumfanya Bwana wetu Yesu kuwa Bwana wa maisha yetu!

## UKIRI WA KINABII

**Mimi ni kiumbe kipya, na akili yangu imebadilishwa kupitia Neno la Mungu. Ninaishi maisha ambayo ni tofauti na ya ulimwengu huu. Haya ndio maisha ya Ufalme! Maisha yangu yamejaa nuru na yamejaa utukufu, kwani nimemfanya Yesu kuwa Bwana juu ya maisha yangu.**

**SOMO LA ZIADA**
Warumi 14: 8-9



**Marko 16:15**
**Akawaambia, Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe.**

Sisi kama Wakristo lazima tutambue kwamba tuko kwenye misheni, na utume huu umefafanuliwa na andiko hapo juu. Tunapaswa kwenda ulimwenguni kote, na agizo lililowekwa ni kuhubiri Habari Njema ya Neema ya Mungu kwa kila mtu! Ndio maana umetumwa katika jamii unayojikuta upo humo leo, iwe mahali pako pa kazi, mahali pa biashara, chuo kikuu chako au nyumbani. Hapo ndipo mahali ambapo unahitaji kuleta athari.

Lazima uwe na ufahamu wa misheni hii ili uweze kuona umuhimu wa kuishi. Hakuna chochote hapa duniani kinachoweza kukutikisa kwa sababu akili yako iko kwenye kusudi hili. Akili yako iko kwenye misheni yako. Usijitenge mbali na kusudi lako kwa sababu mkazo wako ni kwenye vivutio na uharibifu unaoweza kupata katika ulimwengu huu. Zingatia jambo hili moja, KUVUNA NAFSI!

## UKIRI WA KINABII

**Leo nimeweka nia yangu kwenye misheni iliyopo. Ninachagua kuelekeza umakini wangu sio kwa kile ulimwengu huu unaweza kunipa, lakini katika kuhubiri Habari Njema ya Neema ya Mungu katika jamii yangu. Nimeandaliwa na kuagizwa. Nimewezeshwa na Roho Mtakatifu katika Jina la Yesu!**

**SOMO LA ZIADA**
Mithali 11:30; Matendo 1: 8



**Waebrania 5:13**
**Kwa maana kila mtu atumiaye maziwa hajui sana neno la haki, kwa kuwa ni mtoto mchanga.**

Haki ni asili ya Mungu ambayo ilipewa roho yako ulipozaliwa mara ya pili. Inakupa uwezo wa kusimama mbele za Mungu bila hisia yoyote ya hatia, hukumu au kudharauliwa. Hii inaitwa kusimama kwa haki. Hii ni muhimu kwako kujua kwa sababu ubora wa maisha yako inategemea uelewa wako wa haki yako katika Kristo. Imani yako haiwezi kwenda zaidi ya ufahamu wako wa juu ya haki.

Andiko hapo juu linatuonyesha kuwa wale ambao bado wanatumia maziwa huchukuliwa kama watoto kiroho. Kwa watoto wachanga kiroho tunaweza kusema, "Mungu atakuponya." Ingawa hii inaweza kuwa kweli, ni kwa wale tu ambao hawana ujuzi katika Neno la haki. Waliokomaa kiroho wanajua zaidi; wanaishi katika afya ya kiungu. Hawamngoji Mungu kwa ajili ya uponyaji. Hawamsihi Mungu kwa ajili ya uponyaji. Wanajua jinsi ya kutumia Neno na kuishi katika Neno. Wanatumia Neno kudhibiti kila hali, na wanashinda dhidi ya shida zote. Ni lazima ukue katika Neno! Kuwa mtaalamu wa kulitenda Neno, mwenye kugawanya Neno la Kweli!!

## UKIRI WA KINABII

**Ninaamuru na ninatangaza kuwa kila siku, ninakua katika Neno la Mungu. Neno la Mungu linazalisha ubora na utukufu. Nimewekwa kwenye maisha ya ushindi kupitia Neno. Mimi ni mtendea kazi wa Neno katika Jina la Yesu.**

**SOMO LA ZIADA**
Yakobo 1:22; 1 Wakorintho 13:11; Wagalatia 4: 1



**1 Wakorintho 6:17**
**Lakini yeye aliyeungwa na Bwana ni roho moja naye.**

Kitu cha ajabu sana kilitokea ulipozaliwa mara ya pili! Wakati huo, mara moja ukawa kiumbe kipya. Ukawa tofauti kabisa na "wewe" yule wa zamani ambaye hakuzaliwa mara ya pili. Kwa maneno mengine, ukawa kiumbe kipya cha kipekee.

Haukuletwa tu katika maarifa ya Kristo, lakini ulilelwa katika umoja na Kristo. Ni muhimu kujua kwamba sasa mmekuwa roho moja ambayo haiwezi kutenganishwa kabisa na Roho wa Bwana.

Wewe sasa ni mmoja na Mungu! Wewe si mwanadamu wa kawaida tena, kwa maana maandiko yanasema sasa ni washiriki wa asili yake ya Kiungu.

## UKIRI WA KINABII

**Asili na utukufu wa Kristo viko ndani yangu. Kwa hivyo, nina kile Anachosema ninacho, na ninaweza kufanya kile Anachosema ninaweza kufanya. Hakuna mazingira au hali ambayo haiwezi kushindwa kwangu, kwa sababu niko ndani ya Kristo, na ushindi wangu umehakikishiwa ndani Yake. Mimi ni mmoja na Mungu; Mimi ni utukufu wake kama vile Yeye alivyo utukufu wangu, katika Jina la Yesu.**

**SOMO LA ZIADA**
Wakolosai 2:10; 1 Yohana 5:20; 2 Petro 1: 4



**Wakolosai 2: 9**
**Maana katika yeye unakaa utimilifu wote wa Mungu, kwa jinsi ya kimwili.**

Ukiishika kweli hii leo, hautashindwa kamwe kwa chochote unachoweka akili yako kukifanya. Katika andiko hapo juu, tunagundua kwamba utimilifu, ujumla ya uungu, ulikuwa unakaa katika mwili wa Yesu. Ikimaanisha, wakati Yesu alitembea duniani, uungu wote ulikuwa nyumbani kwake. Alikuwa Mungu aliye hai, akitembea na kuzungumza katika mwili wa mwanadamu. Kwa kweli, Mtume Paulo alisema hivi, "ilimpendeza Baba kwamba ndani yake [Yesu] utimilifu wote ukae" (Wakolosai 1:19). Je! Unaona hilo?Sasa, hapa ndipo inashangaza zaidi. Wakolosai 2:10 inasema, "Nanyi [mimi na wewe] tumekamilika katika Yeye [Yesu Kristo]." Sasa neno "kamili" hapo linamaanisha ujazo kamili, kufanywa kamili! Umejazwa na yule yule ambaye Yesu amejaa naye. Utukufu kwa Mungu! Je! Unaona hii? Hii inamaanisha Uungu una nyumba yake ndani yako. Unambeba Mungu kokote uendako! Unawezaje kushindwa wakati ujumla wa Mungu umekufanya makao yake?Kama Yesu, wewe pia ni makao ya uungu. Hii ilitokea lini? Hii ilitokea wakati Roho Mtakatifu alikuja maishani mwako ulipozaliwa mara ya pili! Alileta ndani yako jumla ya Uungu wote!

## UKIRI WA KINABII

**Nimejaa Mungu! Mungu yu ndani yangu; Anatembea ndani yangu; Anaongea ndani yangu. Kwa hivyo, mimi sio mtu wa kawaida. Yeye aliye ndani yangu ni mkuu kuliko yeye aliye ulimwenguni. Ulimwengu uko chini ya miguu yangu, na ninatembea katika njia ya ushindi na mafanikio, katika Jina la Yesu!**

**SOMO LA ZIADA**
Yohana 14: 9; Wakolosai 2:10



**Zekaria 10: 1**
**Mwombeni BWANA mvua wakati wa masika, naam, BWANA afanyaye umeme, naye atawapa manyunyu ya mvua, kila mtu atapewa nyasi kondeni.**

Inaweza kunyesha kwa kila mtu isipokuwa wewe. Wakati wako wa kutembelewa unaweza kukupita wakati unasubiri fataki. Kamwe sio mwanga, kamera, matendo na Mungu lakini sauti ndogo tulivu inayokuongoza.Zaburi 102 aya ya 13 inasema, "Utasimama, na kuirehemu Sayuni, kwa maana ndio wakati wa kuihurumia, naam, majira yaliyoamriwa yamewadia." Mwaka huu fanya kitu thabiti ambacho kinathibitisha wewe ni nani na nini unaweza kufanya. Kuwa mshangao na maajabu. Wakati wako uliowekwa ni sasa, na huu ni wakati wako wa neema.

Wakati sahihi wa kiroho unategemea umakini wako wa kiroho. Patikana katika Neno na uwe katika maombi, na hutaukosa msimu wako. Chukua muda wa kusikiliza sauti hiyo. Andika maono chini na uyababdike ukutani. Yaweke mbele yako na uyaone kila wakati mbele yako. Atamia juu yake katika tafakari za kila wakati, yatamkie na kuyaimarisha katika maombi. Kabla hujajua, wakati wako utafika, na wakati huo ni sasa.

## UKIRI WA KINABII

**Wakati wangu uliopangwa ni sasa. Niko macho kiroho, na kila kitu kimejipanga pamoja kwa ajili ya kufanikiwa kwangu.**

**SOMO LA ZIADA**
Habakuk2:3



**1 Petro 2:24**
**Yeye mwenyewe alizichukua dhambi zetu katika mwili wake juu ya mti, tukiwa wafu kwa mambo ya dhambi, tuwe hai kwa mambo ya haki; na kwa kupigwa kwake mliponywa.**

Ni vyema kuponywa na kuumwa kote au ugonjwa wowote, lakini vipi kuhusu kutokuwa mgonjwa kamwe? Kwa kweli hiyo ni bora zaidi, na ndio maisha ambayo Yesu alileta; maisha ya afya ya kiungu.Afya ya kiungu kwa Mkristo sio ahadi; ilikuja kama sehemu ya kifurushi cha wokovu. Ni sehemu ya matokeo na athari ya uzima wa milele ndani yako. Biblia inasema, "Na huu ndio ushuhuda, ya kwamba Mungu alitupa uzima wa milele, na uzima huu umo katika Mwanawe" (1 Yohana 5:11).
Kwa wewe kuzaliwa upya, una uzima wa milele, na uzima wa milele hauitaji uponyaji. Kwa hivyo, haijalishi ni nini kinashambulia mwili wako. Ikiwa utachochea maisha ya Mungu katika roho yako, mwili wako wote utatunzwa. Maandiko yanasema, "ikiwa Roho wake Yeye aliyemfufua Kristo Yesu katika wafu anakaa ndani yenu, Yeye aliyemfufua Kristo Yesu katika wafu ataihuisha nas miili yenu iliyo katika hali ya kufa kwa Roho wake anayekaa ndani yenu" (Warumi 8:11).

## UKIRI WA KINABII

**Nashuhudia kwamba nimempokea Mwana wa Mungu, Yesu Kristo. Kwa hivyo, nina maisha ya Mungu. Maisha hayo ambayo hayawezi kukumbukwa na hayawezi kuathiriwa na maumivu, kuumwa, magonjwa au udhaifu. Maisha hayo yanapita kwenye utu wangu, yakiupa uzima mwili wangu kila siku. Nashuhudia kwamba, katika Kristo, ninastawi katika afya ya kiungu.**

**SOMO LA ZIADA:** Wagalatia3:13; Wakolosai2:15; Yohana14:12-14



**Yohana 16:13**
**Lakini yeye atakapokuja, huyo Roho wa kweli, atawaongoza awatie kwenye kweli yote.........**

1 Wakorintho 2 mistari 9 hadi 12 inasema, "Lakini kama ilivyoandikwa, Mambo ambayo Jicho halikuyaona, wala sikio halikuyasikia, (wala hayakuingia katika moyo wa mwanadamu,) Mambo ambayo Mungu aliwaandalia wampendao. Lakini Mungu ametufunulia sisi kwa Roho wake....... mambo ya Mungu hakuna ayafahamuye mtu, ila Roho wa Mungu. Lakini sisi hatukuipokea roho ya dunia, bali Roho atokaye kwa Mungu; makusudi tupate kuyajua tuliyokirimiwa na Mungu. "

Kuna vitu ambavyo tumepewa bure na Mungu, na Roho Mtakatifu hufunua kwetu na kutusaidia kufurahia. Hakuna mtu aliye na Roho Mtakatifu anapaswa kamwe kutembea katika giza au sintofahamu. Yeye ni nuru ya uzima. Kupitia nuru yake, unaona yote ambayo Mungu amekubariki, na unaweza kutembea katika nuru ya urithi wako katika Kristo.

## UKIRI WA KINABII

**Roho Mtakatifu ndiye Mwalimu na Kiongozi wangu. Amenijaza hekima ya kushughulikia vyema maishani, akinipa uelewa wa uhalisia wa kiroho. Nimepokea ufahamu zaidi juu ya mafumbo na siri za maisha yangu mapya katika Kristo.**

**SOMO LA ZIADA**
Yohana 14:26; 2 Petro 1: 20-21; 1 Wakorintho 2: 9-12



**Matthew 5:14**
**Ye are the light of the world. A city that is set on a hill cannot be hid.**

Katika kitabu cha Yohana, sura ya 9, aya ya 5, tunagundua kwamba Yesu alijiita Nuru; "Muda nilipo ulimwenguni, mimi ni nuru ya ulimwengu." Sasa, katika Mathayo, Yeye anakuita kile alichojiita mwenyewe. Alisema, wewe ni nuru ya ulimwengu.

Hii inatupa muono wa ndani juu ya kusudi letu hapa duniani. Tumeitwa kuangazia giza lililozungka ulimwengu wetu. Wewe ni nuru ya ulimwengu wako kwa njia ile ile ambayo Yesu alikuwa Nuru ya ulimwengu. Ndivyo ulivyo! Kama mwanafunzi, wewe ndiye nuru katika shule yako. Kama mfanyabiashara, wewe ndiye taa ya tasnia yako. Kazini kwako, Wewe ni nuru huko pia. Basi nuru yako iangaze na kuwavuta watu katika maarifa kamili ya Yesu!

## UKIRI WA KINABII

**Nimewekwa kiungu kama nuru, na lazima niangaze katika ulimwengu huu. Kupitia mimi, wale ambao hawajaokolewa katika ulimwengu wangu watasikia na kupokea nuru ya Injili, na kubadilishwa na kugeuzwa kutoka gizani kwenda kwenye nuru, kwa Jina la Yesu.**

**SOMO LA ZIADA**
1 Timotheo 1: 11-12; 2 Wakorintho 5: 18-19; Yohana 8:12



**Warumi 6:23**
**Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti; bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu.**

Mara tu ulipozaliwa mara ya pili na kumpokea Roho Mtakatifu, ulipokea maisha na asili ya Mungu. Wokovu haukuishia tu na msamaha wa dhambi na kuingia Mbinguni. Ulipokea uzima wa milele, ambao ni asili ya Mungu. Yesu alitoa maisha yake kwa ajili yetu ili tuweze kuishi na kutembea katika haki yake, utukufu, na neema. Haleluya! Leo shikilia ukweli huu: kuzaliwa mara ya pili ni kuwa na maisha ya Kristo yaliyowekwa kwenye roho yako ili uwe hai kwa Mungu, naye akae ndani yako! Utukufu kwa Mungu!Kama Mkristo, amka na ukweli kwamba una maisha na asili ya Mungu ndani yako.

## UKIRI WA KINABII

**Ninathibitisha kwamba Yesu Kristo ndiye Bwana wa maisha yangu, na maisha yake na asili yake vimewekwa kwenye roho yangu. Nimehuishwa kwenye ubaba wa Mungu, na ninaelezea haki ya Mungu katika ulimwengu wangu. Kwa hivyo, kufeli hakumo ndani yangu, kwa maana ninatembea katika utimilifu wa Utukufu Wake, katika Jina la Yesu.**

**SOMO LA ZIADA**
1 Yohana 5: 11-13; 2 Wakorintho 5:21



**Warumi 8:37**
**Lakini katika mambo hayo yote tunashinda, na zaidi ya kushinda, kwa yeye aliyetupenda.**

Haijalishi unakabiliwa na hali gani. Inaweza kuwa matokeo mabaya shuleni, hali ngumu kazini, au maumivu mwilini mwako. Hata ikiwa umepokea habari hasi, au mambo hayaonekani kuwa katika namna ulivyotaka, endelea kudumisha mwelekeo wako kwenye Neno na kile Neno linasema juu yako.

Unamkumbuka Yusufu? Alikaa katika Neno licha ya nyakati ngumu alizokutana nazo huko Misri. Alishtakiwa kwa ubakaji, akatupwa gerezani kwa uhalifu ambao hakufanya, lakini aliendelea kufokasi. Kwa wakati uliofaa, aliinuka kutoka kuwa mfungwa na kuwa waziri mkuu kwa ghafla kabisa (ona Mwanzo 41: 39-44). Kuwa kama Yusufu. Shikilia kile Mungu amesema juu yako katika Neno Lake na ukatae kukata tamaa.

## UKIRI WA KINABII

**Licha ya ugumu na nyakati ngumu ninazoweza kukumbana nazo, ninakubali uwepo wa Neno maishani mwangu, na nachagua kudumisha mwelekeo wangu kwa kile Bwana amesema juu yangu kupitia Neno.**

**SOMO LA ZIADA**
1 Petro 2:15

# Imani Inaweza Kuhamisha Mlima



**Marko 11:22**
**Yesu akajibu, akamwambia, "Mwaminini Mungu.**

Katika andiko letu la leo, tunaambiwa tuwe na Imani ya namna ya Mungu, imani isiyo ya kawaida ambayo Mungu hutumia. Tunamuona akitumia kanuni hii ya imani katika Mwanzo 1. Dunia ambayo Mungu aliumba ilikuwa imeharibiwa na ilifunikwa na giza kuu. Alitumia imani kukileta katika mwili kile ambacho alikuwa amekipata katika ulimwengu wa roho.

Kwa kutumia kanuni hiyo hiyo ya imani, unaweza kuunda tena au kuumba upya ulimwengu wako. Unaweza kuleta mambo mazuri ambayo unataka kuyaona katika maisha yako. Uwezo wa kufanikisha jambo hili upo kwnye Neno la Mungu kinywani mwako. Kama ambavyo Mungu aliumba ulimwengu kwa kutumia Neno Lake, tengeneza maisha yako leo. Tumia imani ya namna ya ki-Mungu!

## UKIRI WA KINABII

**Roho wa Mungu ameniingiza katika nafasi ya mafanikio ya kudumu ambapo kila kitu kimeamriwa kufanya kazi pamoja kwa faida yangu. Kila mahali niendako, na katika kila kitu ninachofanya, nafanikiwa kwa kupiga hatua kubwa.**

**SOMO LA ZIADA**
Waebrania 11: 1



**Mwanzo 1:26**
**Mungu akasema, Na tumfanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu; wakatawale samaki wa baharini, na ndege wa angani, na wanyama, na nchi yote pia, na kila chenye kutambaa kitambaacho juu ya nchi.**

Mungu alipokuwa akimuumba Adamu, Biblia inasema alimfanya kwa mfano wake na sura yake, ili afanane na kutenda au kufanya kama Mungu. Alitaka Adamu awe nakala ya kaboni ya Yeye mwenyewe hata kufikia hatua ya kumjaribu Adamu ili kuona ikiwa atafanya na kutenda kama Yeye. Mungu aliumba wanyama na ndege na kuwaleta kwa Adamu ili kuona ikiwa atawaita haswa kama kile alichokuwa ameamua kuwaita. Adam aliwapa majina yote sahihi, na ilithibitika kwa Mungu kwamba Adamu alikuwa kopi yake bora.Unaona, Mungu alikusudia sisi sote tuwe kama Yeye. Wakati Adamu alipoanguka, Mungu alimfanya Yesu achukue nafasi yake, na Yeye (Yesu) akawa Adamu wa pili. Alimfanya Yesu kuwa mfano Wake halisi (ona Waebrania 1: 3). Kama ulipompokea Yesu kama Bwana na Mwokozi, sasa anaishi ndani yako na anakusaidia kufanyika sura ya Mungu. Hiyo inamaanisha una nguvu ya Mungu ndani yako kufanya kazi kama Yeye na kuyaita mambo ambayo hayako kama vile yamekuwa. Una nguvu ya kubadilisha maisha yako na kuumba kwa maneno yako, kama vile Mungu alivyoumba kwa kutumia Neno Lake. Leo elewa kuwa umeumbwa kwa mfano wa Mungu na ubadilishe maisha yako kwa maneno yako unapoanza kufanya kazi kama Yeye.

## UKIRI WA KINABII

**Ninaachilia neno ili kuumba maisha yangu ya baadaye. Nimewezeshwa kutenda na kufanya kazi kama Mungu kwa sababu ya Kristo ndani yangu.**

**SOMO LA ZIADA:** Wakolosai 1:15



**Waebrania 4:10**
**Kwa maana yeye aliyeingia katika raha yake amestarehe mwenyewe katika kazi yake, kama vile Mungu alivyostarehe katika kazi zake.**

Wakristo wengi wanaonekana kuwa katika mbio za panya. Wanafanya kazi kwa bidii, hata kufanya kazi hadi mfupa ili tu waweze kumudu na kufurahia anasa za maisha. Lakini nina habari njema. Unaona, kama watu wa namna ya Mungu aliye mwema, hatukupaswa kufanya kazi hadi tuanguke. Biblia inasema kwamba tumeingia katika pumziko la Mungu. Tumeacha kazi. Ametupatia vitu vyote tunavyohitaji kwa ajili ya maisha na utauwa. Hakuna taabu zaidi ambayo mimi na wewe tunapaswa kufanya hivi sasa ili kufurahia faida za ulimwengu huu wa mwili au kiroho.Katapausis inamaanisha kupumzika, hali ya heri ambayo Mungu anaishi na ambapo unakoma kuteseka kwa kazi. Imani yako ni hali ya kupumzika. Amini katika kukupatia kwake mahitaji na wema wake unaofanya kazi katika maisha yako, na ruhusu Neno Lake libadilishe ulimwengu wako. Unaingia katika pumziko Lake unaposikia Neno Lake na kulitumia kwa imani. Leo usisikie tu Neno. Lishike kwa imani na anza kuona ulimwengu wako ukibadilishwa.

## UKIRI WA KINABII

**Neno linanifanyia kazi. Imani yangu ni thabiti, na ninafurahia faida za pumziko Lake, kwa jina la Yesu.**

**SOMO LA ZIADA**
Waebrania 4: 2



**BECOME A UAF PARTNER TODAY BY VISITING**

**WWW.UEBERTANGELFOUNDATION.ORG**

UEBERTANGEL
FOUNDATION





**Ayubu 23:10**
**Lakini yeye aijua njia niendeayo; Akisha kunijaribu, nitatoka kama dhahabu.**

Metali zote hubadilika rangi vikipita kwenye moto. Dhahabu tu ndio itatoka ikiang'ara zaidi. Kamwe huwezi kusema ipi ni halisi na ipi ni feki mpaka vitakapojaribiwa kwenye moto. Metali bora kuliko zote huonekana wakati ikiwa motoni.

Haijalishi shetani anakutupia nini, yanakusudia kuyaibua yailiyo bora kutoka kwako. Biblia inasema kwamba ikiwa shetani angejua, asingemsulubisha Bwana wetu kwa sababu mambo hayakwenda kama vile alivyofikiria.

Nina habari njema kwako. Haijalishi unapitia Mungu atasababisha vitu vyote kwa pamoja kuwa kwa faida yako. Ninaona njia yako inang'aa na kung'aa kuelekea siku yako njema!

## UKIRI WA KINABII

**Haijalishi moto Ibilisi ananitupia, natoka nje bila hata kujeruhiwa kwa utukufu wa Mungu. Vitu vyote vinafanya kazi kwa faida yangu kwa Jina la Yesu!**

**SOMO LA ZIADA**
Warumi 8:28



**Zaburi 91: 4**
**Kwa manyoya yake atakufunika, Chini ya mbawa zake utapata kimbilio; Uaminifu wake ni ngao na kigao**

Kulingana na andiko letu la leo, Mungu atakufunika kwa manyoya yake, na chini ya mbawa zake utahifadhiwa. Kwa hivyo, usiogope ajali, mashambulizi ya kigaidi, magonjwa au sunami kwa sababu Baba yako wa mbinguni anakupenda na anakulinda.

Njia mojawapo ambayo Huitumia ni pamoja na malaika zake. Mungu ametangaza kuwa hakuna maovu, tauni au ajali itakayokupata au hata kukaribia makao yako, kwa kuwa atawaamuru malaika zake wakulinde katika njia zako zote. Anaposema hakuna chochote, hakuna chochote! Na ikiwa anawaambia malaika zake wakulinde katika njia zako zote, inamaanisha ulinzi wa kiungu masaa yote kwako!Baba yako wa mbinguni anakulinda. Ndiyo sababu hakuna mabaya yatakayokupata, wala tauni yoyote haitakuja karibu na makazi yako. Na ana jeshi la malaika kukulinda katika njia zako zote leo!

## UKIRI WA KINABII

**Bwana ndiye kimbilio langu na nguvu za maisha yangu. Ninalindwa na Mungu, na sitaogopa kwa Jina la Yesu.**

**SOMO LA ZIADA**
Matendo 4:12



**3 Yohana 1: 2**
**Mpenzi naomba ufanikiwe katika mambo yote na kuwa na afya yako, kama vile roho yako ifanikiwavyo.**

Watoto wengi wa Mungu wanadanganywa na kuamini kwamba kuwa maskini ni ishara ya unyenyekevu wakati ni ishara wazi kwamba uko nje ya mapenzi ya Mungu juu ya maisha yako. Sikiza, umasikini sio mpango wa Mungu kwako. Uliumbwa kuishi maisha mazuri na kufurahia mema ambayo ulimwengu huu unatoa.Bwana Yesu mwenyewe alisema kwamba alikuja ili mpate kuwa na uzima na kisha muwe nao tele. Ninaweza kukuhakikishia, kwamba maisha hayakujumuisha umaskini. Daudi alikuja kugundua ukweli huu aliposema, "Bwana ndiye Mchungaji wangu, sitapungukiwa na kitu" (Zaburi 23: 1). Kwa maneno mengine, mradi Bwana yu pamoja nami, sitapungukiwa. Alijua kwamba maadamu Mungu yuko pamoja naye, hatakuwa mhitaji kamwe.

Ndugu na dada, sasa kwa kuwa mmekuja kwa Kristo, ustawi huja nayo. Huwezi kujizuia zaidi ya kuwa sumaku ya pesa. Ni kosa kwako kuishi katika umasikini. Umewekwa kufanikiwa, na hakuna chochote kitakachokuzuia! Unabeba uwezo wa kuwa tajiri zaidi ya mawazo na fikra zako za mbali zaidi. Nenda na ukafanikiwe leo!

## UKIRI WA KINABII

**Ustawi ni urithi wangu, kwa Jina la Yesu! Nimepokea neema ya kupata utajiri, na hakuna pepo Duniani au Kuzimu atakayenizuia. Sitafilisika siku nyingine yoyote maishani mwangu!**

**SOMO LA ZIADA**
2 Wakorintho 8: 9



**Kutoka 3:14**
**Mungu akamwambia Musa, MIMI NIKO AMBAYE NIKO; ………"**

Changamoto yoyote ile uliyonayo leo hii, iwe ya kimwili, ya kihisia, ya kifedha au ya ndoa, Niko Ambaye Niko anakutangazia kuwa Mimi ni Niko kwako kama unavyohitaji niwe. Vitu vyote vinawezekana kwa Mungu. Je! Unahitaji uponyaji? Anasema, "Mimi ndimi Bwana nikuponyaye" (Kutoka 15: 26). Kwa kupigwa kwake uliponywa. Pokea uponyaji wako hivi sasa katika Jina la Yesu! Je! Unapapasa gizani, wala hujui la kufanya? Yeye ndiye Mpanga mikakati wa Ajabu, Mshauri wa Ajabu. Unaweza kutumia faida ya hekima Yake.

Je! Unashangaa ikiwa kuna zaidi ya maisha kuliko kuishi tu siku hadi siku? Anasema, "Mimi ndiye ufufuo na uzima." Alikuja kukupa uzima. Na palipo na uzima, hakuwezi kuwa na kifo. Una maisha na maisha kwa utele zaidi. Haijalishi ni changamoto gani maisha yananakupa leo; unachohitaji kinapatikana kwa Yesu. Yeye ni msaada tele wakati wa mahitaji.

## UKIRI WA KINABII

**Bwana ndiye Mchungaji wangu. Sitapungukiwa kitu chochote kizuri. Ana uwezo wa kufanya mengi kupita yote na zaidi ya yote ambayo ningeweza kuomba au kuwaza.**

**SOMO LA ZIADA**
Waefeso 3:20



**Waefeso 3: 19**
**na kuujua upendo wake Kristo, upitao ufahamu kwa jinsi ulivyo mwingi, mpate kutimilika kwa utimilifu wote wa Mungu.**

Kujawa na Mungu ni kujazwa na kila kitu ambacho ni Mungu kwako na anacho kwa ajili yako. Kujawa na Mungu ni kuja mahali pa maisha, afya, amani, wingi, na mema yote kabisa. Mungu alipokuumba, alikubuni wewe kuenenda kwa kiwango bora ukiwa umejazwa na upendo wake, kama gari linaloenda vyema linapojazwa na aina sahihi ya petroli au au mafuta. Unapogundua ni jinsi gani Mungu anakupenda na unajazwa pendo lake kwako, utajazwa kiungu na utimilifu wa Mungu.

Biblia inatuambia kwamba Mungu mwenyewe ni pendo. Na unapoanza kutembea katika upendo, na unajua upendo wake kwako, unaanza kutembea katika asili ya kiungu ya Mungu. Ndugu na dada, unapoanza kutembea katika upendo, utapata baraka kubwa za Mungu zitakazokuwa zikilipuka katika maisha yako! Utakuwa sumaku ya baraka!

## UKIRI WA KINABII

**Pendo la Mungu limemiminwa moyoni mwangu na Roho Mtakatifu. Ninakataa kutembea kwa hofu na hatia. Nimekubalika kwa Mpendwa. Haleluya!**

**SOMO LA ZIADA**
1 Yohana 4: 8, 16



**Isaya 43: 1**
**Lakini sasa, BWANA aliyekuhuluku, Ee Yakobo, yeye aliyekuumba, Ee Israeli, asema hivi, Usiogope, maana nimekukomboa; nimekuita kwa jina lako, wewe u wangu.**

Mungu anakujali sana kiasi kwamba hata nywele za kichwa chako zimehesabiwa. Anajua wakati nambari 233 itaanguka. Muumba wa Mbingu na Dunia, Yeye aliyeweka nyota angani, Yeye anayedumisha ulimwengu kwa neno Lake, Mungu huyo huyo anakujua sana!Anajua si tu jina lako, lakini pia anajua kila kitu kukuhusu. Hakuna hali katika maisha yako ambayo hupita bila Yeye kuijua. Yeye sio mjinga kwa Habari ya shida zako, lakini yupo nawe na anataka kubadilisha hali yako.Uwe na hakika leo. Mungu yule yule aliyekuumba hajasahau kukuhusu. Anakujua kwa jina lako. Jina lako limeandikwa katika kiganja cha mkono Wake. Mungu hajakusahau. Anakupenda!

## UKIRI WA KINABII

**Bwana yu pamoja nami siku zote; Siwezi kamwe kuwa peke yangu. Na leo, nachagua kutwika fadhaa zangu zote, kwani ananijali. Haleluya!**

**SOMO LA ZIADA**
Luka 12: 7



**Yohana 10:11**
**Mimi ndimi mchungaji mwema. Mchungaji mwema huutoa uhai wake kwa ajili ya kondoo**

Mungu anatamani kukuelekeza na kukuongoza katika changamoto za maisha ya kila siku. Kama mwamini, haupaswi kamwe kujisikia mnyonge kwa sababu Mchungaji Mwema anakuongoza kila wakati. Yeye ndiye anayekuongoza na kukutunza vizuri wewe pamoja na biashara zako. Huenda mbali zaidi na kuongoza kila hatua unayochukua.

Bwana ndiye Mchungaji wako; hutapungukiwa. Kwa hivyo, chochote kinachoonekana kinakosekana kwa leo, anza kusema na hali hiyo kwamba Bwana ndiye Mchungaji wako, na ukosefu hauna nafasi katika maisha yako. Kwa hivyo katika kila kitu unachofanya leo, fikiria kwamba Bwana Mungu yuko kukuongoza kuelekea mafanikio yako, kuinuliwa kwako.

## UKIRI WA KINABII

**Leo najua hakika kwamba Bwana ndiye Mchungaji wangu binafsi. Ananielekeza na kuniongoza kuelekea mafanikio yangu. Sitapungukiwa kitu chochote kizuri.**

**SOMO LA ZIADA**
Zaburi 23: 1



**2 Wakorintho 3:18**
**Lakini sisi sote, kwa uso usiotiwa utaji, tukiurudisha utukufu wa Bwana, kama vile katika kioo, tunabadilishwa tufanane na mfano uo huo, toka utukufu hata utukufu, kama vile kwa utukufu utokao kwa Bwana, aliye Roho.**

Wakati wowote unapojitazama kwenye kioo ili ujione mwenyewe, na unapojiangalia kwenye kioo cha Neno la Mungu, utakuwa ukiangalia kile Mungu alikuumba wewe kuwa. Hiyo inaweza kuwa sio ukweli wako wa wakati huu, lakini unapoendelea katika Neno, tazama utukufu wa yule aliyefanikiwa ndani yako.

Unabadilishwa kutoka kushindwa hadi kufanikiwa. Hii haikamiliki kwa bidii yako yoyote ya kufanikiwa maishani, lakini kwa Roho wa Bwana! Wewe ndiye uliyeumbwa kudhihirisha utukufu wa Mungu. Ndio maana ukiangalia kwenye kioo cha Neno la Mungu, unaona utukufu wa Mungu. Unapojitazama katika Neno la Mungu leo, unabadilishwa kutoka magonjwa kwenda afya, kutoka umasikini hadi ustawi, kutoka masononeko hadi furaha isiyoelezeka.

## UKIRI WA KINABII

**Ninabadilishwa kutoka utukufu kwenda utukufu kwa Jina la Yesu. Ninapoangalia katika habari njema, ninatoka na ushuhuda!**

**SOMO LA ZIADA**
Zekaria 4: 6



**Zaburi 23: 5**
**Waandaa meza mbele yangu, Machoni pa watesi wangu. Umeni-paka mafuta kichwani pangu, Na kikombe changu kinafurika.**

Moja ya majina ya Mungu wetu ni Yehova Jireh, ambayo inamaanisha Yeye anayetoa mahitaji yote. Yeye hutoa zaidi ya ya kutosha. Ndio maana Daudi anasema katika andiko letu la leo, kikombe changu kinafurika. Ali-kuwa na uzoefu wa Mungu wa zaidi ya kutosheleza.Nina habari njema kwako leo kwa sababu Mungu wetu ni yeye yule jana, leo, na hata milele na milele. Alichomfanyia Daudi, atak-ufanyia pia. Ona moyo wa Mungu kwa ajili yako leo. Anataka kukufaniki-sha. Usikubaliane na chochote kidogo, ukifikiri kwamba Yeye anakupa tu ma-hitaji yako na sio matakwa yako.Ikiwa unahitaji kazi, ujue Yeye anataka uombe sio kwa ajili ya kazi tu bali pia kwa cheo. Unapokuwa na cheo, una ushawishi, na una uwezo wa kuathiri maisha. Labda unachohitaji ni nyongeza ya mshahara. Basi omba sio hiyo tu, bali pia uwe katika nafasi ya kutoa ongezeko.

## UKIRI WA KINABII

**Bwana ndiye Mchungaji wangu. Sitapungukiwa kitu chochote kizuri. Namtumikia Mungu wa zaidi ya kutosheleza. Haleluya!**

**SOMO LA ZIADA**
Waefeso 3:20



**1 Wakorintho 1:27**
**bali Mungu aliyachagua mambo mapumbavu ya dunia awaaibishe wenye hekima; tena Mungu alivichagua vitu dhaifu vya dunia ili aviaibishe vyenye nguvu;**

Kamwe usivunjwe moyo na watu ambao wanakuambia jinsi huna sifa au kutostahili kwa kile unachotaka kwani Mungu amebobea katika kuwastahilisha wasio na sifa za kustahili. Andiko letu la leo linatuambia kwamba Hutumia vitu dhaifu kuvidhalilisha wenye nguvu. Hiyo inamaanisha wakati wowote unapojiona umezidiwa idadi na unahisi kutostahili, umekuwa tu mtu sahihi kwa Mungu kuonyesha nguvu zake.

Mungu anaweza kutumia chochote ulicho nacho leo kufanya muujiza katika maisha yako. Mungu wetu Mtaalam wa hali zisizowezekana, kwa hivyo furahia na shangilia. Anakaribia kujionyesha Mwenye nguvu kwa niaba yako.

## UKIRI WA KINABII

**Ninaweza kufanya mambo yote katika Kristo anitiaye nguvu. Mimi ni zaidi ya mshindi. Siku hii ni yangu, kwa Jina la Yesu!**

**SOMO LA ZIADA**
Yoeli 3:10



**Wakolosai 1:13**
**Naye alituokoa katika nguvu za giza, akatuhamisha na kutuingiza katika ufalme wa Mwana wa pendo lake;**

Ninapozungumza na waumini wengi siku hizi, kitu cha kwanza wananiambia ni shida ngapi shetani anawapa na jinsi wanavyohitaji ukombozi. Kwa mujibu wa andiko letu la leo, hii haipaswi kuwa hivyo. Angalia inasema kweli ni Yeye "alitukomboa" kutoka kwenye nguvu za giza, "alitukomboa" ni katika wakati uliopita. Haendi kufanya; tayari imefanywa. Tayari umeondoka mahali hapo pa ukandamizaji, na sasa umesimama katika Ufalme wa Mwana wa Pendo lake, Haleluya.

Shida hutokea wakati unapoanza kutangatanga mbali na mahali pa uhuru wako. Najua unajiuliza ninafanyaje hili? Ni kwa maneno yanayotoka kinywani mwako. "Mgongo huu unaniua!" "Mambo ni magumu kwangu." Unarudi kwenye utumwa kwa maneno yako. Azimia siku hii kusema tu kile Mungu anasema juu yako. Hauzuiliki, umebarikiwa kupita kipimo, Haleluya!

## UKIRI WA KINABII

**Kuumwa na magonjwa havina nafasi ndani yangu. Mimi ni mshiriki wa asili ya ki- Mungu. Ustawi ni wangu katika Jina la Yesu, na vitu vyote vinafanya kazi pamoja kwa faida yangu.**

**SOMO LA ZIADA**
2 Wakorintho 8: 9



**Isaya 29: 16**
**Ninyi mnapindua mambo; Je! Mfinyanzi ahesabiwe kuwa kama udongo; kitu kilichofinyangwa(kilichobuniwa) kimnene yeye aliyekifinyanga (aliyekibuni), Hakunifinyanga huyu; au kitu kilichoumbwa kimnene yeye aliyekiumba, Yeye hana ufahamu?**

Watu wengi hawaelewi nguvu ya mawazo au fikra wanazoruhusu katika akili zao. Kuna mchezo wa maneno katika maandiko yetu ya leo ambayo yanaonyesha nguvu ya mawazo yako. Neno la Kiebrania lililotafsiriwa kama framed kwa kingereza ni yatsar, ambayo inamaanisha kutengeneza au kubuni dhana, fikra au taaswira kichwani. Tunaweza kusoma andiko kama, "Je! Kitu kilichobuniwa (yatsar) kitasema juu ya Yeye aliyekibuni (yatsar), hakuwa na ufahamu?" Uwezo wako wa kufikiria ni uwezo wako wa uumbaji. Unapoanza kutafakari juu ya Habari Njema ya neema Yake, jione mwenyewe katika maandishi ya unachokitafakari.Haijalishi umeshindwa mara ngapi kabla kwenye ndoa yako, shule au biashara. Unaporuhusu Habari Njema kuifanya upya akili yako, mawazo yako yanaweza kuyarekebisha maisha yako ya baadaye kuwa sawa. Hivi ndivyo unavyoingia katika maisha yako ya baadaye kabla ya kuyafanya yaingie ndani yako. Jione mahali unataka kuwa.

## UKIRI WA KINABII

**Ninateka nyara kila fikira ili ipate kumtii Kristo. Afya ya Kiungu ni sehemu yangu, na kufanikiwa ni urithi wangu. Ninahamia katika maisha yangu ya baadaye sasa, kwa Jina la Yesu.**

**SOMO LA ZIADA**
Waebrania 2:18



**Zaburi 1: 3**
**Naye atakuwa kama mti uliopandwa Kandokando ya vijito vya maji, Uzaao matunda yake kwa majira yake, Wala jani lake halinyauki; Na kila alitendalo litafanikiwa**

Hakuna mtu aliyezaliwa katika ulimwengu huu aliyekusudiwa na Mungu kuwa maskini, mgonjwa, aliyevunjika moyo, aliye na huzuni, aliyekatishwa tamaa au mwenye shida. Badala yake, mapenzi ya Mungu ni kwa watu wote kufanikiwa na kuwa na afya, kama roho zao zinavyofanikiwa (3 Yohana 1: 2). Mungu anataka ufanikiwe katika roho yako, nafsi yako, na mwili wako, na ndio sababu hupaswi kukaa au kukubali magonjwa, umaskini, au kushindwa.

Ustawi huu, hata hivyo, ni zaidi ya pesa. Uwepo au ukosefu wa pesa haubadilishi hali yako au kiroho chako, na kwa hivyo haifai kubadilisha ushuhuda wako wa Mungu. Pesa ni chombo. Kilicho muhimu ni nguvu ya ununuzi, na nguvu yako ya ununuzi sio pesa; ni imani yako! Wewe ni kile Mungu anasema wewe ni, bila kujali sarafu ulizonazo mikononi au la.

## UKIRI WA KINABII

**Vitu vyote ni vyangu. Siwezi kamwe kuwa duni. Ninaishi kwa imani ya Kristo, na vitu vyote vinawezekana.**

**SOMO LA ZIADA**
Wagalatia 2:20



**Zaburi 91: 15**
**Ataniita nami nitamwitikia; Nitakuwa pamoja naye taabuni, Nitamwokoa na kumtukuza;**

Wakati Paulo aliambiwa na Roho Mtakatifu kwamba vifungo na mateso yalimngojea, Paulo alisema, "Lakini siyahesabu maisha yangu kuwa kitu cha thamani kama kuumaliza mwendo wangu na huduma ile nimepokea kutoka kwa Bwana Yesu, kuishuhudia Habri Njema ya neema ya Mungu," (Matendo 20:24).

Unapojua kuwa Mungu yuko pamoja nawe, hakuna chochote kitakachoweza kukuhamisha. Adui anaweza kutupa ngumi yake bora, lakini wakati vumbi litakapotulia, utakuwa bado umesimama. Simama imara leo, ukijua kuwa hatakuacha kamwe wala kukutelekeza.
Tayari umeshinda. Ushindi wako katika Kristo hauwezi kujadiliwa; ni jambo la uhakika. Haijalishi unakabiliwa na changamoto gani leo, ahadi ya Mungu ni kwamba atakuwa pamoja nawe katika shida. Kwa hivyo kamwe usikate tamaa; ushindi ni wako.

## UKIRI WA KINABII

**Ninamshukuru Mungu wangu kuwa siko peke yangu, kwani yuko pamoja nami siku zote. Nina Mpanga mikakati wa Ajabu ambaye ndiye mshauri wangu katika maswala yote ya maisha. Siwezi kuzuia zaidi ya kufanikiwa leo!**

**SOMO LA ZIADA**
Yohana 14:18


H. E. AMBASSADOR UEBERT ANGEL
ONLINE
PROPHETIC
SEMINAR
SEPT 29 - OCT 1
IN 3 DAYS:
1) LEARN TO PROPHESY ABOUT INTERNATIONAL EVENTS
2) LEARN TO SEE IN THE SPIRIT REALM AND AVOID THE HINDRANCES TO SEEING SPIRITUALLY
3) RECEIVE DIRECT IMPARTATION FOR DEEPER PROPHETIC UNCTION
SIGNUP NOW ON WWW.UEBERTANGEL.ORG

OSBORN INSTITUTE of THEOLOGY



# ENROL NOW
## FOR SUMMER INTAKE
### CERTIFICATE & DIPLOMA

THE OSBORN INSTITUTE OF THEOLOGY FOUNDED BY PROPHET UEBERT ANGEL AND FULLY ACCREDITED BY TRANSWORLD ACCREDITING COMMISSION INTERNATIONAL, PROVIDES AN AWARD-WINNING ONLINE LEARNING PLATFORM THAT EQUIPS MEN AND WOMEN WITH THE REVEALED WORD OF GOD. OIT PREPARES MEN AND WOMEN TO SHARE AND BEAR WITNESS OF JESUS CHRIST TO THE CHURCH AND THE WORLD.

ACADEMIC EXCELLENCE · TRANSWORLD ACCREDITING COMMISSION INTERNATIONAL · EDUCATION · ACCOUNTABILITY

ENROL NOW AT WWW.OSBORNINSTITUTE.COM



**Waebrania 4: 1**
**Basi, ikiwa ikaliko ahadi ya kuingia katika raha yake, na tuogope, mmoja wenu asije akaonekana ameikosa.**

Katika Biblia yote, utapata maandiko yakikuambia, "Usiogope." Lakini andiko letu la leo ni la kipekee. Hii ni moja ya nyakati adimu unazoambiwa uogope kitu. Kuwa na hofu kwamba huenda usiingie katika rahani mwa Mungu. Kuna jambo moja tu ambalo litakuzuia kutoka kwenye raha hii, nalo ni kutokuamini. Kushindwa kuamini kwamba Mungu anakupenda kutakufanya usisite kumtwika Mungu matatizo yako.Mpango wa Mungu kwako ni kuishi maisha ya raha. Kuingia katika raha yake ni uamuzi wa ufahamu. Wakati unapumzika, haujali chochote. Unaweza kupumzika ukijua kuwa sio lazima ukabiliane na shida zako peke yako. Mungu anashirikiana nawe katika shida zako. Lakini lazima ushiriki katika pumziko lako. Amini kwamba Mungu anakujali. Matatizo yanapokujia, kataa kuyabeba kama mzigo. Kwa haraka iwezekanavyo, kwa imani, yatupie kwa Mungu kupitia maombi. Yeye ndiye mdakaji wako anayeweza. Na linapokuja suala la matatizo yako, hatakosa kamwe, na Yeye hatayaachilia.

## UKIRI WA KINABII

**Ninashirikiana na Mtatuzi wa Matatizo, na ninakataa kutishwa na wasiwasi wa maisha haya. Hakuna undani juu ya maisha yangu ambao Mungu utampita asiujue. Anajihusisha na yale yanayonihusu. Ana uwezo, na ananijali; kwa hivyo, nitapumzika.**

**SOMO LA ZIADA**
1 Petro 5: 7



**Matendo 3: 6**
**Lakini Petro akasema, "Mimi sina fedha, wala dhahabu, lakini nilicho nacho ndicho nikupacho......"**

Haiwezekani kwako kutoa kile ambacho haujapokea. Katika Matendo sura ya 3, Petro alipokutana na yule kiwete, aliweza kutoa nguvu ya Mungu ya kuponya. Alipokea nguvu hiyo akiwa katika maombi. Katika Marko sura ya 4, Yesu alijikuta katikati ya dhoruba. Walakini alikuwa amejiachia sana, alikuwa amelala usingizi mzito juu ya mto. Alipoamka, Akaachilia pumziko, na dhoruba ikatulia. Aliweza kutoa kile alichokuwa amepokea katika maombi. Maombi ni mahali pa kupokea kile unachohitaji.Kamwe huwezi kutuliza dhoruba wakati wewe mwenyewe haujatulia. Lazima kwanza upokee amani kabla ya kuiachilia katika maisha yako mwenyewe na mazingira yako. Katika ulimwengu wa Roho, unapokea na kuachilia kwa maneno. Yesu alisema, "Amani yangu nawapa." Ameachilia kile Alichopokea. Sehemu yako ni kupokea, kwa imani, amani ambayo ameiachilia. Kisha, kwa imani, iachilie kwa kutangaza amani yake kenye mazingira yako na hali ya maisha yako.

## UKIRI WA KINABII

**Ninapokea amani ya Mungu. Amani yake inalinda akili yangu dhidi ya mawazo ya kuleta wasiwasi. Nina nia ya Kristo. Kwa hivyo, akili yangu imetulia, ina uwiano mzuri, na haina shaka, wasiwasi, au hofu. Ninatamka amani kwenye mwili wangu, fedha, kaya, na yote yanayonihusu katika Jina la nguvu la Yesu.**

**SOMO LA ZIADA**
Yohana 14:27; 2 Wakorintho 4:13



**1 Timotheo 1:18**
**Mwanangu Timotheo, nakukabidhi agizo hilo liwe akiba, kwa ajili ya maneno ya unabii yaliyotangulia juu yako, ili katika hayo uvipige vile vita vizuri;**

Unashiriki katika vita, lakini hii sio vita ya nguvu. Ni vita ya mkakati. Ibilisi hana nguvu, ila maneno tu. Maneno yanaweza kushindwa tu na maneno yaliyo bora zaidi. Unapopokea neno la kinabii kutoka kwa Bwana, unakuwa umekabidhiwa silaha ambayo inaweza kukatakata na kupiga neno lolote ulilonong'onezwa kutoka kwa shetani, baba wa uwongo. Vidonda pekee ambavyo vitaachiliwa vitakuwa juu ya adui, sio kwako wewe.

Yesu alikuwa bwana wa kutumia silaha ya kinabii juu ya maisha yake. Alifuata maandiko ya kinabii na alikataa kumruhusu adui amzuie. Mungu pia ametangaza Neno la kinabii juu ya maisha yako. Amesema kuwa mipango yake ni kukufanikisha. Hiyo ndiyo silaha yako. Unaposhambuliwa katika eneo linalohusu ustawi wako, toa silaha yako. Jikumbushe unabii na utangaze neno ulilopokea kutoka kwa Bwana. Tangaza unabii, na utilie shaka mashaka yako. Unapotilia shaka mashaka yako, hiyo ndiyo imani. Na imani katika Neno la kinabii ulilopokea ni silaha ambayo inashinda kila wakati.

## UKIRI WA KINABII

**Mimi siwezi kufishwa. Maadamu jukumu langu halijaisha, sishindwi. Ninafanikiwa katika afya yangu, katika akili yangu, na katika fedha zangu. Ustawi ni hatima yangu ya kinabii, na hakuna silaha iliyoundwa dhidi yake itafanikiwa.**

**SOMO LA ZIADA**
Yeremia 29:11; Waebrania 10: 7



**2 Wakorintho 9:10**
**Na yeye ampaye mbegu mwenye kupanda, na mkate uwe chakula, atawapa mbegu za kupanda na kuzizidisha, naye atayaongeza mazao ya haki yenu;**

Maisha ni ya kiroho. Kila kitu kina mizizi ya kiroho, ikiwamo pesa. Mara nyingi watu hufanya makosa kuomba ili wapate pesa. Lakini pesa hazitii maombi. Inafuata sheria na kanuni, sheria za kiroho. Sheria ya kiroho ambayo inasimamia pesa haikuruhusu kumiliki kile unachokataa kukigawa. Kama Mungu hawezi kuipata kupitia wewe, basi Haiwezi kuileta kwako. Unapoendesha mambo kwa Roho, na kukaa katika sheria za Roho, basi una amri ya kiungu juu ya kile kinachodhibitiwa na Roho.

Ili Mungu akuamini na pesa, unahitaji kuwa mrija wa usambazaji. Hiyo inafanya ustawi wako wa kifedha uwe rahisi kama maamuzi. Elewa kuwa kama mtu wa kiroho, unayo haki na mamlaka ya kudhibiti mambo ya kiroho. Pesa ni kitu cha kiroho ambacho kinaweza kudhibitiwa tu na mtu wa rohoni. Amua kuwa mtu huyo. Badala ya kusubiri mtu akupe, amua kuwa mtoaji, na Mungu wa wingi atahakikisha rasilimali zako za kifedha zinapatikana kila wakati.

## UKIRI WA KINABII

**Mimi ni kamanda wa himaya wa pesa. Mimi ni mtoaji na msambazaji wa pesa. Ninadhibiti pesa kutokea ulimwengu wa roho. Kwa hivyo, sitapungukiwa rasilimali.**

**SOMO LA ZIADA**
Mwanzo 12: 2-3; Wagalatia 3: 13-14



**Luka 6:45**
**Mtu mwema katika hazina njema ya moyo wake hutoa yaliyo mema, na mtu mwovu katika hazina mbovu ya moyo wake hutoa yaliyo maovu; kwa kuwa mtu, kinywa chake hunena yale yaujazayo moyo wake.**

Hapa kuna hadithi kwa ajili yako. Punda alianguka ndani ya kisima. Alipojua kuwa alikuwa amenaswa, alilia kwa masaa. Kwa kadri alipokuwa akilia, ndivyo alivyozidi kuzama chini zaidi. Mgeni anayepita aliangalia chini kisimani, na aliona punda huyo hakuwa na thamani ya kuokolewa. Aliamua kusukumia mavumbi juu ya punda ili kumuondolea shida anayoipata. Punda alipogundua kuwa alikuwa anazikwa akiwa hai, alilia zaidi. Baada ya muda, aligundua hali ilikuwa inazidi kuwa mbaya, aliamua kutulia. Badala ya kulia, ilianza kutikisa kila lundo la mavumbi juu yake na kuyatumia kukijaza kisima kwa mavumbi yale mpaka akafanikiwa kutoka nje ya kisima.Maisha yako leo ni matokeo ya maneno uliyoyazungumza jana. Maneno yaliyotumiwa vibaya yanaweza kuwa mtego kwako. Ndio sababu ni bora kuwa mtu wa maneno machache kuliko kusema maneno mabaya ambayo yanaweza kukuzika ukiwa hai. Wakati hali za maisha zinaonekana kukutupia mavumbi, usilie juu yake. Badala yake, tumia maneno yako kubadilisha mazingira yako kuwa bora. Ikiwa maneno mabaya yamekuingiza kwenye mtego, haujachelewa kugeuza mambo. Tulia. Chagua maneno yako kwa uangalifu, na uyatumie kujiimarisha maishani.

## UKIRI WA KINABII

**Mimi ndiye msanifu wa maisha yangu, na maneno yangu ndio ramani ambayo ninatumia kujenga. Hivi sasa, ninapozungumza, ninainuliwa kwa kiwango kingine. Upendeleo unaongezeka katika maisha yangu. Shida zangu zinaajiriwa kwa kuinuliwa kwangu. Kushindwa kwangu ni mpango mkakati wa mafanikio yangu. Ninainuka juu ya kila hali kwa sababu nguvu ya ufufuo inafanya kazi ndani yangu. Haleluya!**

**SOMO LA ZIADA:** Mithali 6: 2; Yakobo 3:10



**Maombolezo 3: 22-23**
**Ni huruma za BWANA kwamba hatuangamii, Kwa kuwa rehema zake hazikomi. Ni mpya kila siku asubuhi; Uaminifu wako ni mkuu.**

Mwanzoni mwa mwaka huu, nilitoa wimbo wa kiroho kwa ajili ya ulinzi wako na malaika kuwa karibu nawe. Unaposikiliza wimbo huo, unatengeneza mazingira ambayo yamejaa uwepo wa Mungu. Wewe pia umepewa jukumu la kutoa nyimbo. Mtunga Zaburi anatuambia kwamba tunapaswa kumwimbia Bwana wimbo mpya. Hiyo inamaanisha una uwezo, uwezeshwaji wa kuandika nyimbo za kuabudu kwa Bwana. Unapoandika wimbo, unaandika barua ya mapenzi kwa Mungu. Unapoandika nyimbo za Mungu, andika tu juu yake, sio juu yako, kwa sababu katika ibada, kila kitu kinamuhusu BWANA.Biblia inatuambia kwamba rehema za Bwana ni mpya kila asubuhi. Ikiwa unaimba kuhusu rehema mpya za Mungu kila siku, unapaswa kuwa na angalau nyimbo mpya 365 kila mwaka. Anza sasa. Kila siku, mwimbie Bwana kwa rehema zake. Haijalishi ikiwa wewe ni mwimbaji mzuri au ikiwa unaweza kufanya tu ni kelele za shangwe. Mungu anataka uupe huba moyo wake. Huna haja hata ya kuunda maneno. Chukua andiko kutoka kwa Neno la Mungu na utumie kutengeneza mashairi yako. Weka hali ya siku yako kwa wimbo wa kuabudu kwa Mpenzi wa roho yako.

## UKIRI WA KINABII

**Mimi ni mwabudu. Kuabudu ni asili yangu, utamaduni wangu, na mfumo wangu wa maisha. Ninatengeneza mazingira ya ukaribu na undani ambapo Mungu huadhimishwa, kuheshimiwa, na kuhusudiwa.**

**SOMO LA ZIADA**
Zaburi 89: 1; 96: 1



**Warumi 12: 2**
**Wala msiifuatishe namna ya dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza, na ukamilifu.**

Kuna namna ya kuinua akili yako ili kila wazo liwe katika makubaliano kamili na Roho wa Mungu. Inaitwa kufanya upya nia yako. Mwekezaji anapochukua umiliki wa rasilimali mpya, ikiwa kilicho ndani ya rasilimali hiyo hakikidhi kiwango au ubora unaohitajika kwa mmiliki mpya, hufanyiwa marekebisho. Katika ukarabati, unaondoa yote yaliyopitwa na wakati na yale yenye ubora wa chini, na kubadilishia na vilivyo bora zaidi. Ikiwa kitu kimevunjika, unakitengeneza. Ikiwa chochote kinakosekana, unarejeshea kipya. Kila kitu ambacho mwekezaji hufanya ni nia ya kuongeza thamani ili iweze kumfaa mmiliki mpya. Ulipozaliwa mara ya pili, maisha yako yalikuwa chini ya umiliki mpya. Roho Mtakatifu alifanyika Mwekezaji wa maisha yako. Namna ulivyokuwa unafikiria haikufaa tena. Akili yako ilifanyiwa ukarabati, na nyenzo bora zinazohitajika kufanya maboresho ni Neno la Mungu. Unapoingia katika Neno, mawazo yako ya zamani yanabadilishwa, na kila kitu kukuhusu kinaboreshwa.

## UKIRI WA KINABII

**Akili yangu inainuliwa na Neno la Mungu. Ninapambanua mambo kwa kiwango cha juu. Sina shaka, hofu, au kuchanganyikiwa, kwa sababu Neno la Mungu linashinda vyote katika maisha yangu.**

**SOMO LA ZIADA**
Wafilipi 2: 5-6



**1 Wakorintho 15:10**
**Lakini kwa neema ya Mungu nimekuwa hivi nilivyo; na neema yake iliyo kwangu ilikuwa si bure, bali nalizidi sana kufanya kazi kupita wao wote; wala si mimi, bali ni neema ya Mungu pamoja nami.**

Ninaposoma maandiko kama aya ya leo, ninaamshwa katika roho yangu! Hii inatuambia kitu kikubwa. Kila kitu ambacho ni wewe na kila kitu utakachokamilisha ni matokeo ya neema. Wewe pia, kama Paulo, unaweza kutamka, "kwa neema ya Mungu, nimekuwa hivi nilivyo!" Yesu ndiye NIKO Ambaye NIKO. Chochote alicho, kwa neema ya Mungu, ndivyo wewe ulivyo katika ulimwengu huu. Kweli hii ikiwa na mizizi ndani ya roho yako, siku zako za kusumbuka zimekwisha!

Paulo anasema, nilifanya kazi kwa bidii kuliko nyote mkijumuishwa pamoja. Lakini ni jambo linalofuata alilosema linalotupa kitu cha kushangilia kwa sauti. Anasema, lakini sio mimi niliyekuwa nikifanya kazi. Ilikuwa neema ya Mungu pamoja nami! Haleluya! Neema ni mwajiriwa wako, mfanyakazi mwenzako. Jukumu likiwekwa mbele yako, ujue kuwa sio lazima ulifanye peke yako. Neema iko pamoja nawe na inakufanyia kazi! Tangaza neema hiyo juu ya miradi yako na juu ya kila jambo, na angalia Mungu alifanya maajabu kwako

## UKIRI WA KINABII

**Ninakataa kujisumbua! Jitihada zangu zote zinaungwa mkono na neema ya Mungu. Ninafanikiwa katika yote ninayofanya, kwa sababu neema inafanya kazi ndani yangu, kwa ajili yangu, na pamoja nami! Utukufu kwa Mungu!**

**SOMO LA ZIADA**
Wagalatia 2:20



**Wimbo wa Sulemani 5:16**
**Ndiye mzuri sana..........**

Je! Umewahi kukutana na mtu ambaye hajui jinsi ya kuchukua pongezi? Unawaambia jinsi mavazi yao yanavyooneka vizuri, na mara wanakujibu kwa kukuambia ni ya zamani kiasi gani. Unawapongeza juu ya kitu, na wanaonyesha kitu kingine ambacho wanaona kama kasoro. Labda wewe ni mtu kama huyo. Lakini ikiwa ni hivyo, leo ni siku ya mwisho ambayo unajidharau.Biblia inatuambia kwamba mawazo ya Mungu juu yetu ni mazuri. Lazima uelewe kwamba mawazo yake ni ya juu sana. Hakuna mawazo ya juu kuliko Yake. Na ikiwa anasema kwamba Yeye anafikiria tu mawazo mazuri juu yako, ni nani atakuwa na ujasiri wa kutosha kupinga hilo? Ikiwa anakuwazia mema tu, huna haki ya kufikiria padogo juu yako. Badili mawazo yako leo kuhusu wewe ni nani. Sahau juu ya ulikotoka au kile ulichofanyiwa hapo zamani. Kuanzia wakati huu, anza kusema tu kile Mungu anasema juu yako. Na ujue kuwa kila kitu Anachosema juu yako ni nzuri.

## UKIRI WA KINABII

**Aliye Mkuu yuko ndani yangu. Kwa hivyo, mimi ni mkuu. Mimi ndiye ambaye Mungu anasema mimi niko. Nimejaa hekima. Mimi ni kiongozi sokoni. Mimi ni mtu wa ushawishi. Nina ujasiri, siogopi, na ninajiamini. Kila kitu Yeye yuko, na mimi ndivyo nilivyo!**

**SOMO LA ZIADA**
1 Yohana 4:17



**Warumi 5: 8**
**Bali Mungu aonyesha pendo lake yeye mwenyewe kwetu sisi, kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu, tulipokuwa tungali wenye dhambi.**

Hiyo ni moja ya mistari inayokomboa zaidi katika Biblia kwa sababu inakujulisha kuwa uhusiano wako na Mungu unategemea neema yake. Kristo alikufa kwa ajili yako ulipokuwa katika hali mbaya na hujali hochote kuhusu Yeye. Kwa kweli, Biblia inasema wewe ulikuwa adui yake, umetengwa nje ya ushirika na urafiki na Yeye. Walakini alikupenda vya kutosha hata kutoa maisha yake kwa ajili yako. Ni jambo la busara kwamba ikiwa haukuhitaji kufanya chochote ili Yeye akupende, hauitaji kufanya chochote ili Yeye aendelee kukupenda. Hiyo ndiyo maana ya neema.Unaweza kufadhaika sana sasa hivi kwa sababu unajaribu "kumpendeza Mungu" kulingana na matendo yako mema. Ni muhimu kwako kuelewa kuwa haki, au kusimama sawa na Mungu, hakutegemei wewe kusoma Biblia vya kutosha, kuomba kwa kutosha, kwenda kanisani vya kutosha, kutoa zaka ya kutosha, au kufanya chochote vya kutosha. Neema haina uhusiano wowote na kile unachofanya, matendo yako. Inategemea tu yale ambayo Yesu amekufanyia tayari, na hiyo ni habari njema.

## UKIRI WA KINABII

**Mimi ni mwenye haki kabisa, ninapendwa kabisa, na mtakatifu kabisa, sio kwa sababu mimi natenda kikamilifu, lakini kwa sababu mimi ndiye mpokeaji wa neema kamili ya Mungu.**

**SOMO LA ZIADA**
Wakolosai 1: 20-21



**2 Wakorintho 10: 4-5**
**(maana silaha za vita vyetu si za mwili, bali zina uwezo katika Mungu hata kuangusha ngome;) tukiangusha mawazo na kila kitu kilichoinuka, kijiinuacho juu ya elimu ya Mungu; na tukiteka nyara kila fikira ipate kumtii Kristo;**

Ngome ni mbaya kuliko udanganyifu. Ni rahisi kuzungumza na mtu na kumtoa kwenye ukengeufu. Lakini ngome inakuwa mtazamo, sehemu ya wewe ni nani. Inakuwa namna yako ya maisha. Ngome zinaweza kuwa mawazo fulani, maneno, misemo, au mambo hasi unayosema juu yako. Elewa kwamba maneno ni vitu. Unaporuhusu akili yako kuishi juu yake, au kuyazungumza katika anga, yanakua umbo. Ndio maana wazo baya linapokuja ndani ya kichwa chako, lazima uliharibu mara moja. Kuna njia moja tu ya kubomoa ngome, na hiyo ni kwa kupata Neno la kutosha ndani yako. Ukijaa Neno, Neno ndani yako litajibu kila wazo lisilosahihi. Biblia inaita hii "kuangusha chini" fikra au mawazo ambayo yanakwenda kinyume na mapenzi ya Mungu juu maisha yako. Kuangusha chini kunamaanisha uko katika kiwango cha juu. Kamwe usishuke kwenye kiwango cha mawazo hasi. Jiweke katika hali ya kujazwa na Neno. Kaa kwenye kiwango chako, na angusha chini kila mawazo hasi.

## UKIRI WA KINABII

**Mimi ni mtendaji wa Neno. Akili yangu imejazwa na Neno la Mungu. Kwa hivyo, nafikiria kama Mungu anavyofikiria. Nimeketi pamoja na Kristo katika ulimwengu wa roho, na ninakataa kupunguza kiwango changu kwa mawazo hasi.**

**SOMO LA ZIADA**
Waefeso 2: 6



**Mithali 4: 20-22**
**Mwanangu, sikiliza maneno yangu; Tega sikio lako, uzisikie kauli zangu. Zisiondoke machoni pako; Uzihifadhi ndani ya moyo wako. Maana ni uhai kwa wale wazipatao, Na afya ya mwili wao wote.**

Neno la Kiebrania kwa "afya" katika kifungu hiki ni marpé , ambalo linamaanisha 'dawa' au 'tiba.' Neno la Mungu ni wakala wa dawa kwa mwili wako, mwili wako wote, ndani na nje. Kwa kweli, unaye Mtaalam ambaye anajua kila undani wa mwili wako kutoka kichwa hadi wayo wako. Katika Kutoka 15, aya ya 26, Anasema, "Mimi ni Bwana nikuponyaye." Ilitafsiriwa kutoka kwenye Kiebrania cha asili, inamaanisha "mimi Bwana ndiye daktari wako." Yeye ni Jehova Rapha. Rapha sio neno la kiroho. Ni neno la Kiebrania linalomaanisha 'daktari wa matibabu.' Mungu ni daktari wako, na dawa anayokuandikia ni Neno Lake. Biblia inasema kwamba Neno la Mungu ni afya kwa mwili wako WOTE. Haijalishi ikiwa ni chunusi kwenye uso wako au uvimbe wa saratani ndani ya mwili wako. Neno ni maagizo ya kuponya na kuganga magonjwa yako yote. Kama vile kumeza vidonge, Neno hufanya kazi vizuri linapomezwa ndani. Lisome. Litafakari. Lizungumze mpaka ujue kwa kina ndani ya ufahamu wako kwamba limeufikia mwili wako. Kamwe huwezi kuzidisha dozi yake, kwa hivyo limeze kwa kadri unavyoweza. Kadiri unavyolimeza Neno Lake, ndivyo utakavyokuwa bora zaidi.

## UKIRI WA KINABII

**Mwili wangu uko chini ya usimamizi wa Neno la Mungu. Kila seli katika mwili wangu inaitikia wakala wa uponyaji wa Neno. Maisha yananijia sasa! Afya inanijia sasa! Kifo kimeondolewa kutoka kwenye mwili wangu, na ninapokea uponyaji wangu kwa Jina la Yesu!**

**SOMO LA ZIADA:** Warumi 8:11; Yohana 8: 31-32



**Wafilipi 4: 8**
**Hatimaye, ndugu zangu, mambo yo yote yaliyo ya kweli, yo yote yaliyo ya staha, yo yote yaliyo ya haki, yo yote yaliyo safi, yo yote yenye kupendeza, yo yote yenye sifa njema; ukiwapo wema wo wote, ikiwapo sifa nzuri yo yote, yatafakarini hayo.**

Ikiwa unatazama televisheni na kitu kinakuja ambacho hautaki kuona, unabadilisha tu idhaa. Vivyo hivyo, kama kuna kitu ambacho unataka kutazama, unabadilisha idhaa na kugeukia kile unachotaka kuona. Hivyo ndivyo Mtume Paulo anakuambia ufanye katika aya ya leo.Kama vile antenna kwenye runinga yako, akili yako ni king'amuzi cha hali ya juu. Hivi sasa, kuna kila aina ya mawimbi yanayorushwa ambayo akili yako ina uwezo wa kuyafungulia. Mawimbi haya huja kwa njia ya mawazo, mengine mazuri na mengine maovu. Ni juu yako kuamua kuyafungulia mawazo yale ambayo ni mazuri. Neno la Mungu linasema, fikiria juu ya mambo ya kupendeza. Kwa maneno mengine, ikiwa wazo halikunufaishi, lizime. Akili yako imeundwa kwa ajili ya mawazo bora ambayo ni mema kwako na mazuri kwa kiwango cha juu zaidi.

## UKIRI WA KINABII

**Akili yangu ni mali isiyohamishika ya bei ghali zaidi. Mawazo tu yanayokidhi vigezo kamili, yenye ubora wa hali ya juu huruhusiwa kufanya makazi. Hakuna uvamizi hasi wanaruhusiwa. Akili yangu imefanikiwa. Maisha yangu yameundwa. Na ninapamanua mambo kwa kiwango cha juu.**

**SOMO LA ZIADA:** 1 Wakorintho 2:16



**Zaburi 16: 6**
**Kamba zangu zimeniangukia mahali pema, Naam, nimepata urithi mzuri.**

Nyumba inapofanyiwa ukarabati, msanifu huletwa kusanifu mipango. Anaona jinsi nyumba inavyopaswa kuonekana haswa na kuandaa michoro ya ramani. Mara nyingi mmiliki wa nyumba hawezi kuona kile msanifu anaona. Mmiliki wa nyumba anaangalia kutoka kwa mlengo wa jinsi nyumba inavyoonekana sasa. Msanifu, hata hivyo, anaangalia kutoka kwenye mlengo wa jengo lililomalizika.

Mungu ana mpango wa maisha yako, mwongozo wa kiungu. Na muundo Wake umejengwa kikamilifu. Unaweza kuwa unaangalia maisha yako na unashangaa ni vipi chochote kizuri kinaweza kutoka kwenye mazingira yako ya sasa. Lakini amini usanifu Wake. Ana ujuzi kamili wa wapi upo na wapi unahitaji kuwapo. Neno la Mungu ndilo malighafi za ujenzi wa maisha yako. Unapoingia katika Neno Lake, unajengwa juu ya msingi wa uhakika. Maisha yako yanaundwa kuwa kitu kizuri. Nataka kukuombea.

## UKIRI WA KINABII

**Ninatamka jambo linalozidi kawaida la ajabu sana kutokea maishani mwako, wimbi jipya, mwonekano mpya, harakati mpya, mwendo mpya. Na kuwepo kujongea kwa vipande ambavyo haviko mahali pake ili kukuweka katika usawa, ili kwamba baraka ambayo haiwezi kubadilishwa ije juu ya maisha yako. Umaskini umefutwa kutoka kwenye maisha yako! Ongezeko ni lako, kwa Jina la Yesu!**

**SOMO LA ZIADA:** Waefeso 4: 15-16



**Isaya 55: 1**
**Haya, kila aonaye kiu, njoni majini, Naye asiye na fedha; njoni, nunueni mle; Naam, njoni, nunueni divai na maziwa, Bila fedha na bila thamani.**

Andiko letu la leo linatujulisha kuwa kuna mazingira, hali ya hewa, ambapo hauhitaji pesa kununua kitu. Kwa kweli unaweza kupata kitu kinachozivuta rasilimali zote unazohitaji. Kwa kweli, unaweza kuwa tajiri. Unachohitaji kufanya ni kulishika na agizo lililowekwa. Mithali 4, aya ya 20 inasema hivi: "Yasikilize maneno yangu; tega sikio lako usikie maneno yangu."

Biblia nzima ni kwa faida yako. Hiyo ndiyo amri iliyowekwa. Lakini kuna sehemu fulani za Neno ambazo ni maalum kwa ajili yako. Unapotaka ukweli juu ya mada fulani, zitafute hizo. Kuna maandiko yaliyotengwa maalumu kukupeleka kule unakotaka kwenda. Tafuta ndani ya Neno kisha ukifuate kitu unachotaka kukipata. Ikiwa unataka uponyaji, tafuta maandiko ambayo yanazungumzia uponyaji wako. Ikiwa unataka kufanikiwa, tega masikio yako kwa maandiko ambayo yanazungumza juu ya ustawi wako. Chochote unachohitaji, kuna maandiko kwa ajili yake.

## UKIRI WA KINABII

**Baraka ya Bwana inanitajirisha bila majuto. Mimi ni mkusanya neema, sumaku ya pesa, sumaku ya rasilimali. Ninajitenga na agizo lililowekwa la ukosefu na umasikini wa kurithi, na ninaishi katika mazingira ya kufanikiwa.**

**SOMO LA ZIADA**
2 Timotheo 2:15



**Wakolosai 4: 2**
**Dumuni sana katika[maisha ya] kuomba, mkikesha katika kuomba huku na shukrani;**

Ikiwa umewahi kumiliki au kuendesha gari mpya, mengi yake yana yanawashwa bila kutumia funguo. Yasiyotumia funguo kuwashwa ni tofauti na magari yale za zamani yanayotumia funguo kuwasha. Kuwasha gari bila funguo hutumia kitu kinachoitwa elektroniki key fob. Huwezi kuwasha injini mwenyewe moja kwa moja, unabonyeza kitufe kuwasha injini badala ya kuchokonoa kwa funguo. Ikiwa hauna fob mahali fulani kwenye gari au kwenye mkoba wako au mfukoni kabla ya kushinikiza kitufe cha kuwasha, gari hilo haliendi popote.

Maombi ni funguo aina ya fob kwa ajili ya maisha yako. Ukiona, vitabu vyangu vingi vinahusu maombi. Unapaswa kuishi maisha ya kuomba, kuwasiliana na Yule umpendaye. Unapoishi maisha ya maombi, una ujasiri mwingi. Bila maombi, unaweza kudhani mambo yanasonga, lakini itafika wakati gari la maisha yako litakwama. Litakuwa likihitaji ufunguo, na ufunguo ni maombi. Maombi na yawe kipaumbele katika maisha yako. Unapoishi maisha ya maombi, utapiga hatua, na mambo yatakuwa rahisi sana.

## UKIRI WA KINABII

**Maombi ni kipaumbele changu. Ninabaki katika ushirika usiobadilika na Bwana. Kwa hivyo, siwezi kukuktwa na jambo bila kujua. Mimi ni Mkristo ninayezalisha uthibisho, na ninaishi maisha ya maendeleo thabiti na ushindi.**

**SOMO LA ZIADA**
Matendo 6: 4

# Ngozi ya Kifaru



**Luka 17: 1**
**Akawaambia wanafunzi wake, Makwazo hayana budi kuja, lakini ole wake mtu yule ambaye yaja kwa sababu yake!**

Jamii zote za faru zina aina tofauti za ngozi. Lakini wote wana kitu kimoja sawa: ngozi yao ni imara na nene. Ngozi ya faru mkubwa iko karibu na sentimita 5 za unene. Lakini pamoja na kuwa ngozi ni nene, faru bado lazima achukue tahadhari kuzuia vimelea vyenye ugonjwa kama kupe. Vimelea vikubwa ambavyo utashughulikia katika maisha yako ya Kikristo ni vimelea vya makosa. Ibilisi atajaribu kutumia makosa kunyonya maisha yako kutoka kwenye furaha na amani yako. Wewe, kama faru, lazima uwe na "ngozi nene" linapokuja suala la makosa.Neno lililotafsiriwa "kosa" ni neno la Kiyunani skandalon, neno ambalo tunapata neno kashfa kwa kingereza. Ni neno linalofananishwa na ndoano ambayo hufyatua mtego wa panya. Labda umesikia msemo, "Yeye anajua kitufe cha kubonyeza," akimaanisha kitu hicho, mara nyingi kitu kinachosemwa, kinachochochea kosa. Mhubiri 7, aya ya 21 inasema, "usitie moyoni mwako maneno yote yaliyosemwa." Unapoona kosa linakuja, tambua hapa ni eneo ambalo shetani anajaribu kukunasa. Usisikilize.Na mama umekisikia, usiyaweke moyoni.Ondoa kitufe cha kosa, ili shetani akose kitu cha kubonyeza.

## UKIRI WA KINABII

**Ninaongozwa na Roho. Sisemi mabaya juu ya mtu yeyote, na sivutwi na maneno mabaya ya wengine. Ninapenda kwa sababu mimi ni mpenzi. Natembea kwa upendo, juu zaidi ya ulimwengu wa kosa.**

**SOMO LA ZIADA**
Mithali 18:19



**1 Wakorintho 3: 3**
**kwa maana hata sasa ninyi ni watu wa tabia ya mwilini. Maana, ikiwa kwenu kuna husuda na fitina, je! Si watu wa tabia ya mwilini ninyi; tena mnaenenda kwa jinsi ya kibinadamu?**

Katika sarufi, kuna kitu kinachoitwa tashbihi. Tashbihi ni tamathali ya semi inaohusisha kulinganisha kitu kimoja na kitu kingine cha aina tofauti. Wakati wowote unaposikia "kama" au "kama vile," hiyo inamaanisha kitu kinachoelezewa kama "kama" au "kama vile" ni tofauti na kitu ambacho kinalinganishwa. Ndio sababu haupaswi kuwa na wasiwasi unaposoma kwamba shetani huenda kama "simba" anayenguruma. Hiyo inakuambia kuwa yeye si s i m b a anayenguruma. Anajifanya tu.

Mstari wetu wa leo unaibua swali lenye nguvu: "Je! Ninyi si wa mwili, na mnaenenda kama watu?" Hiyo inakuambia jambo la muhimu. Mkristo kiumbe kipya hakukusudiwa kutembea "kama" mtu wa kawaida. Mtembeo wako katika Imani ulikusudiwa kuwa wa kiungu. Hauko tena kwa mwili bali katika roho. Amua sasa hivi kwamba matokeo yatakuwa tofauti katika kila eneo la maisha yako. Kristo aliye ndani yako anakupa haki na mpenyo wa maisha yasiyo ya kawaida.

## UKIRI WA KINABII

**Mimi sio wa kawaida. Mimi ni kiumbe kipya katika Kristo, bora kuliko shetani. Nilizaliwa kwa ajili ya ukuu na nimekusudiwa kufanya ushujaa. Nitaweka alama katika ulimwengu huu kwa ajili ya Yesu ambayo haitafutwa kamwe.**

**SOMO LA ZIADA**
Zaburi 82: 6; Warumi 8: 9



**Yohana 8:32**
**tena mtaifahamu kweli, nayo hiyo kweli itawaweka huru.**

Maisha yako yatakwenda kulingana na maarifa, kiwango cha ufunuo ulichonacho. Maarifa uliyokuwanayo kabla ya kuwa Mkristo hayatoshi kukuendeleza mara tu upozaliwa mara ya pili. Wewe mpya unatamani aina tofauti ya lishe. Ni njaa kwa ajili ya kweli. Unaona, kuna tofauti kati ya kweli halisi na kweli iliyothibitishwa. Ukweli uliothibitishwa ni wa asili na unaweza kubadilishwa. Lakini ukweli halisi haubadiliki.

Kama kiumbe kipya, unaishi katika ulimwengu wa kiroho, na ulimwengu huo unadhibitiwa na kweli. Umetumia maisha yako yote kupata maarifa juu ya jinsi ya kuenenda katika ulimwengu huu wa asili. Sasa unahitaji ujuzi wa Neno kuishi katika uwezo wako wa kiroho. Neno la Mungu ni mwongozo wa maisha yako mapya katika Kristo. Ndani yake, utapata habari ambayo inakuambia nini cha kutarajia na jinsi mambo yanahitaji kufanya kazi kwa ajili yako. Utagundua ukweli juu ya wewe ni nani, na ujue ni nini kilicho kwenye jina lako ili uweze kutembea ndani yake.

## UKIRI WA KINABII

**Neno linakua kwa nguvu ndani yangu na kushinda. Mimi sio mnyonge au asiye na matumaini. Siwezi kamwe kuchanganyikiwa au kukosa nafasi, kwa sababu nina Neno la Mungu kwa hali yoyote.**

**SOMO LA ZIADA**
2 Wakorintho 5:17



**Warumi 12: 3**
**.......... kama Mungu alivyomgawia kila mtu kiasi cha imani.**

Imani ni sarafu ya Ufalme ambayo inakupa uwezo wa kuzileta Mbingu Duniani. Sisi sote tumepewa kipimo sawa cha imani. Maandiko yetu kwa leo yanakuwezesha kujua kwamba Mungu aliyomgawia kila mtu kiasi cha imani. Imani yangu haina nguvu kuliko yako. Yote ni juu ya kile unachofanya na imani yako.

Imani inategemea maarifa, taarifa kutoka kwenye Neno la Mungu. Ukipakia roho yako na Neno la Mungu, imani yako haitakuwa inafikika. Imani hufanya kazi kwa sababu Neno lililoko ndani yako, na Neno ndani yako litaitikia hali yako. Imani ni kama misuli. Lazima uitumie ili ikue. Tatizo linapokuja, hiyo sio fursa kwako kuangamizwa. Ni fursa ya kufanyia mazoezi imani yako.

## UKIRI WA KINABII

**Nina imani ya namna ya ki-Mungu inayofanya kazi ndani yangu. Roho yangu imejaa Neno la Mungu, na matatizo yanapoita jina langu, imani inaitikia. Imani yangu inatosha, na haitashindwa.**

**SOMO LA ZIADA**
Waebrania 11: 6



**1 Yohana 5: 14-15**
**Na huu ndio ujasiri tulio nao kwake, ya kuwa, tukiomba kitu sawasawa na mapenzi yake, atusikia. Na kama tukijua kwamba atusikia, tuombacho chote, twajua kwamba tunazo zile haja tulizomwomba.**

Maombi hayafanyiki ili kupata. Maombi hufanywa kwa sababu tayari tumepata. Biblia inasema, "tunajua kwamba tunavyo." Jambo la kwanza unapaswa kujua ni kwamba Yeye anakusikia. Unapohisi umetenda dhambi, una uhakika 100% kwamba Mungu anaona. Walakini unapoomba, hauna hakika kuwa anakusikia. Uwe na hakika, Mungu anakusikia. Unapoomba, inapaswa kuwe na maandishi ya ushindi rohoni mwako kwa sababu hakuna fungu katika Biblia kinachosema Mungu anajibu maombi yako kwa "hapana" au "subiri." Biblia inasema ahadi za Mungu ni ndio na amina. Yeye atakupa haja za moyo wako.

Jifunze kuwasiliana na Mungu. Badala ya kusema unaomba, sema unataka kuzungumza na Mungu. Maombi ni kitu unachofanya kwa sababu unafurahia kuwasiliana na Roho wa uungu. Maombi yanapaswa kuwa matamu sana. Unapoomba,fanya kama unazungumza na mpenzi kwa sababu wewe ni mpenzi. Huisha shauku yako ya maombi, na uombe kama vile hujawahi kuomba hapo awali.

## UKIRI WA KINABII

**Katika mwaka huu wa namna ya Mungu, ninajisogeza karibu na BWANA. Nimerudi kwa mpenzi wangu wa kwanza, na ninafurahia kutumia wakati kuzungumza naye. Miujiza inakuja kirahisi kwangu kwa sababu imezaliwa kutoka kwenye urafiki.**

**SOMO LA ZIADA**
2 Wakorintho 1:20



**1 John 1:3**
**That which we have seen and heard declare we unto you, that ye also may have fellowship with us: and truly our fellowship is with the Father, and with his Son Jesus Christ.**

Nakumbuka wakati mmoja wa wachungaji wangu alipaswa kuwa katika eneo fulani, na alikuwa amechelewa kuwa hapo. Alinipigia simu akasema hazipati funguo zake. Mara moja, katika ulimwengu wa Roho, niliona hakika funguo zake zilikuwa wapi. Nilimwambia, na akaenda moja kwa moja mahali pale na akapata funguo zake. Baada ya kukata simu naye, sikuweza kupata funguo zangu mwenyewe.

Watu wanaweza kupata shida kuamini kwamba siwezi kutumia neema yangu ya kinabii kutafuta funguo zangu zilizopotea hata ingawa nimewatabiria mamilioni ya watu. Linapokuja kwangu, siwezi kutabiri juu ya mahitaji. Lazima nitangaze kwa imani. Unaona, nabii ni zawadi kwa ajili yako. Nabii anaweza kukupa habari, lakini haitafanya kazi kamwe ikiwa hutumii imani yako. Tangaza na utekeleze yale yaliyosemwa juu yako. Rudi kupitia ujumbe huo na uvute kila neno la unabii ambalo ulipewa. Weka Neno kwenye matendo, nalo litafanya kazi.

## UKIRI WA KINABII

**Neema ya kinabii inaongezeka katika maisha yangu. Nina uwezo wa kupokea siri za Ufalme. Ninapoongea, ninaachilia Roho Mtakatifu. Mambo yanasonga, na hakuna maadui watakaoweza kuniharibu hata nifanye nini, kwa Jina la Yesu!**

**SOMO LA ZIADA**
Waefeso 4: 11-12



**Waebrania 10: 7**
**Ndipo niliposema, Tazama, nimekuja (katika gombo la chuo nimeandikiwa) Niyafanye mapenzi yako, Mungu.**

Mtu Wangu wa Mungu, Mchungaji Chris, alikuwa akikaa eneo fulani, na ilitokea moto ndani ya jengo hilo wakati wa usiku. Kila mtu alikimbilia barabarani, wengi wakiwa bado wamevaa nguo zao za kulalia. Wakati ulipita, na Mchungaji Chris alikuwa bado hajatoka nje ya jengo hilo. Ghafla, alitokea, amevaa kawaida kabisa, na akatembea nje bila wasiwasi. Hata jengo linalowaka moto halingemfanya atoke katika tabia yake.

Ufunuo hukufanya ukae katika tabia. Inakuwezesha kujua wewe ni nani. Yesu alisema, "Katika gombo la chuo imeandikwa kuhusu Mimi. Nimekuja kufanya mapenzi yako, Ee Mungu." Alikaa katika tabia. Kamwe usiruhusu chochote kukuondoa kwenye tabia. Wewe ni kila kitu ambacho Neno linasema kuhusu wewe. Biblia inapokuambia kuwa wewe ni tajiri, bila kujali unaona nini kwenye akaunti yako ya benki, kaa kwenye tabia. Kataa kutamka au kutenda umasikini. Biblia ikikuambia kuwa umepona, kaa kwenye tabia. Haijalishi unajisikiaje au vipimo vinasemaje, tangaza uponyaji juu ya mwili wako.

## UKIRI WA KINABII

**Kuanzia taji ya kichwa changu hadi kwenye nyayo za miguu yangu, ninaamuru na kutangaza nimepona! Ongezeko liko juu ya maisha yangu. Pesa zangu zinatoka kila upande. Pesa zinakuja, na pesa zinakaa!**

**SOMO LA ZIADA**
Waefeso 3: 8



**Yohana 5: 5-6**
**Na hapa palikuwa na mtu, ambaye amekuwa hawezi muda wa miaka thelathini na minane. Yesu alipomwona huyu amelala, naye akijua ya kuwa amekuwa hali hiyo siku nyingi, alimwambia, "Wataka kuwa mzima?"**

Yesu alipokutana na mtu huyu, Biblia ilisema kwamba mtu huyo alikuwa hawezi, udhaifu, kwa miaka thelathini na minane. Yesu alikuwa na nguvu wakati huo na mahali pale za kumrudisha huyu mtu katika uuponyaji kamili. Badala yake, anamwuliza mtu huyo swali: "Je! Wataka kuwa mzima?" Kwa nini Yesu aliuliza, unaweza kujiuliza? Ni kwa sababu uzima na mauti viko katika uwezo wa ulimi wako. Unapoongea, unatoa sauti, ambayo husababisha mtetemo. Mtetemo huunda nishati. Nishati huunda mada. Mada inafafanuliwa kama kitu chochote kilicho na tungamo(uzito) na kinachukua nafasi. Kwa hivyo, unaposikia swali, "Una mada gani na wewe?" kinachoulizwa ni nini, ni sauti gani unayoitoa?Kila kitu Duniani kinaongea. Mwili wako unaongea. Pesa yako zinaongea. Mungu anataka uongee. Kuwa na vipindi vya kuongeaa kila siku. Ukiamka usiku, anza kuongea. Ongea mpaka urudi kulala. Unapaswa kuwa na usiku wa kuongea (sio tu maombi ya usiku kucha). Usiongee juu ya vitu hasi. Ongea juu ya jinsi unavyotaka maisha yako yawe. Jiimbie tenzi, ukijitengenezea nyimbo juu ya jinsi ulivyo mkuu. Unapotamka, unapunguza vitu ambavyo sio vya maisha yako, na unajiendeleza kwa kiwango kingine.

## UKIRI WA KINABII

**Nina mtazamo wa yanayowezekana. Ninatumia kinywa changu kwa ajili ya mambo chanya. Kwa maneno yangu, mimi kudhibiti kila kinachonihusu. Ninasukumwa kwenda kiwango kingine. Afya yangu imerejeshwa. Nitakuwa tajiri sana, maadui zangu wote watashtuka.**

**SOMO LA ZIADA:** Yohana 6:63



**Luka 19:13**
**Akaita watu kumi katika watumwa wake, akawapa mafungu kumi ya fedha, akawaambia, Fanyeni biashara hata nitakapokuja**

Kila kitu unachohitaji kuanza biashara kipo katika Neno la Mungu. Neno "tamalaki" katika aya hii haswa linamaanisha "kufanya biashara." Hii haimaanishi huduma. Inahusu biashara ya benki au mfanyabiashara. Mabenki hushughulika na pesa na uwekezaji, na wafanyabiashara hununua na kuuza bidhaa. Hiyo inamaanisha Bwana anatarajia uwe na pesa na uwekeze kwa gawio au faida. Pia anatarajia ushiriki katika ununuzi na uuzaji wa bidhaa au huduma. Kwa kifupi, unahitaji biashara.

Ramani ya mfano wa biashara yako imetolewa katika Mwanzo 1, mstari wa 28:
1. Zaeni. Zalisha bidhaa bora. Unahitaji bidhaa kwanza.
2. Ongezeka. Rudufisha kile unachozalisha na ubora ule ule.
3. Mkatiishe. Jitayarishe kwa ukuaji na uwe na mahesabu.
4. Mkatawale. Dhibiti soko.

Kumbuka kwamba maelekezo ya katika kitabu cha Mwanzo huanza na baraka. Songa mbele kwa kujiamini, kwani Mungu amekupa neema ya kuanza biashara yenye mafanikio.

## UKIRI WA KINABII

**Kila biashara ninayofanya inafanikiwa na kushamiri kama mti wa kijani kibichi kila wakati. Ninapanuka kila upande, nikichukua himaya, na kutawala soko kwa Jina la Yesu!**

**SOMO LA ZIADA**
Mithali 13:22; Kumbukumbu la Torati 8:18



**1 Wakorintho 2: 12-13**
**Lakini sisi hatukuipokea roho ya dunia, bali Roho atokaye kwa Mungu, makusudi tupate kuyajua tuliyokirimiwa na Mungu. Nayo twayanena, si kwa maneno yanayofundishwa kwa hekima ya kibinadamu, bali yanayofundishwa na Roho, tukiyafasiri mambo ya rohoni kwa maneno ya rohoni.**

Kuna msamiati wa kiroho ambao tunautumia. Biblia inasema, " tukiyafasiri mambo ya rohoni kwa maneno ya rohoni" Tunazungumza vitu vya kiroho kwa kutumia msamiati wa kiroho kwa mambo ya kiroho. Shida ni kuwa unazungumza lugha ya kawaida wakati unapaswa kuzungumza kitu ambacho roho zinaelewa.Yesu hakutumia lugha ya kawaida. Ndio sababu aliweza kuzungumza na mtoto aliyekufa ambaye hakuweza kusikia lugha yoyote na kumfufua. Hakuwa anazungumza na vitu. Alikuwa akizungumza na roho. Roho inayoitwa mauti inaelewa lugha yake ya kiroho.Kuna kiwango fulani katika maisha yako wakati ambapo wa kiroho tu huitikia ya kiroho. Kabla ya kunyimwa mkopo katika benki, kuna meneja wa benki wa kiroho. Wakati wowote hali inapokuwa ngumu kwako, inakuwa ni shida ya kiroho inayohitaji mwitikio wa kiroho kwa kutumia msamiati wa kiroho. Unapotaka mambo yasonge, tangaza jinsi unavyotaka hali hiyo ibadilishwe, na unene kwa lugha. Badilisha gia katika Roho. Unaponena kwa lugha, unaachilia moto wa Roho Mtakatifu. Unaweza kuzungumza na roho. Unaweza!

## UKIRI WA KINABII

**Moto wa Roho Mtakatifu umeachiliwa ili kulamba kila mabaki ya ugonjwa kutoka kwenye mwili wangu. Unatoa kila kizuizi na kukifanya majivu. Shida yoyote katika maisha yangu au familia yangu ambayo imenisumbua, jibu ni moto!**

**SOMO LA ZIADA:**Marko 5: 40-42; Yohana 6:63



**Hagai 2: 8**
**Fedha ni mali yangu, na dhahabu ni mali yangu, asema BWANA wa majeshi.**

Huwa mara nyingi nasema mende walikuwa wakija nyumbani kwangu kufunga. Nakumbuka nyuma mwaka 2007, Mungu alisema, "Mwambie mke wako aache kufanya kazi." Wakati huo, tulikuwa na kanisa, na bili zilikuwa zinakuja haraka na hasira. Lakini Mungu akasema, "hizo sio bili zako. Ni bili zangu." Sasa, kila ninapopata bili, ninazishikilia kwa Mungu na kusema, "Kuna bili zako hapa." Unaona, nilishikilia aya ambayo inasema ng'ombe juu ya milima elfu ni wa Mungu. Anamiliki ng'ombe na milima pia. Baba yako ni tajiri kupita ufahamu. Ikilinganishwa na utajiri wa Mungu, Jeff Bezos ni fukara wa kutupwa sana kama mzaha tu.Ikiwa Jezz Bezos hatakuja kupata senti nyingine na atatumia dola milioni moja kila siku, itamchukua zaidi ya miaka 500 kutumia pesa zake zote. Walakini, hakuna mstari hata mmoja kwenye Biblia unaomzungumzia. Wewe, kwa upande mwingine, umeitwa kuwa tajiri. Unapokuwa na wito, kuna mvuto ndani yako. Unapokasirishwa na umasikini wako, hiyo inamaanisha kuna kuvutwa kuelekea ustawi. Panapokuwa na wito, unaanza kufanya vitu ambavyo hukuwahi kufikiria kama utafanya, vitu ambavyo vinapingana na mawazo yako. Umeitwa kufanikiwa. Jibu wito huo.

## UKIRI WA KINABII

**Baba yangu ni tajiri, na mimi nakataa kuwa fukara!**

**SOMO LA ZIADA**
Zaburi 50:10, 12; 2 Wakorintho 8: 9



**Waefeso 1: 22-23**
**akavitia vitu vyote chini ya miguu yake, akamweka awe kichwa juu ya vitu vyote kwa ajili ya kanisa; ambalo ndilo mwili wake, ukamilifu wake anayekamilika kwa vyote katika vyote.**

Mbwa na tembo walikutana. Mbwa alisema, "Nilipata ujauzito na nikazaa. Wewe bado una ujauzito." Wakati walipokutana tena, mbwa alirudia jambo lile lile. Tembo akasema, "Tulia. Ninapozaa kile nilichobeba, dunia itatetemeka. Na watu watakapomwona akija, watakimbia." Ndivyo muujiza wako ulivyo.Usijali juu ya mambo mabaya ambayo mtu yeyote atasema juu ya hali yako. Daima kutakuwa na wasengenyaji, watu ambao hawana chochote kizuri cha kusema. Kuwa na uhakika kwamba unabeba kitu kizuri. Wewe ni ujazo wake yeye anayevijaza vitu vyote katika vyote. Biblia inasema, "Ninyi ni miungu." Anza kuendesha mambo kama mmoja wao. Fikiria, ongea, songa, na ujibu kama mungu.

## UKIRI WA KINABII

**Nina ufahamu wa yanayowezekana. Nina nia ya mafanikio. Nimembeba Mungu, na nimejaa sana kiasi kwamba siwezi kushindwa!**

**SOMO LA ZIADA**
Ufunuo 12:11



**2 Petro 1:19**
**Nasi tuna lile neno la unabii lililo imara zaidi, ambalo, mkiliangalia, kama taa ing'aayo mahali penye giza, mwafanya vyema, mpaka kutakapopambazuka, na nyota ya asubuhi kuzuka mioyoni mwenu.**

Tunayo neno la unabii la uhakika zaidi, ambalo ni Neno la Mungu. Hata kama nabii hatazungumza nawe, Mungu atazungumza nawe kutoka kwenye Neno Lake. Nabii anaweza kuchagua kutokuzungumza nawe. Lakini hakuna mtu anayeweza kumzuia Mungu asiseme nawe. Hiyo ndiyo inayafanya maombi kuwa muhimu sana.Maombi sio monolojia. Ni mjadala. Ndio maana biblia inasema kesha na uombe. Hiyo inamaanisha, unapoomba, pata muda kwa roho yako kumsikia. Unanena kwa ndimi, na anajibu kwa Roho Wake. Lakini huwezi kusikia jibu hilo mpaka ujue Neno la Mungu. Atakuangazia andiko moja kichwani mwako. Wakati mwingine atakupa mawazo ya moja kwa moja. Sio muhimu kwako kumsikia Mungu jinsi ninavyomsikia kama nabii. Kuwa wewe. Omba, kesha, na umsikie Mungu mwenyewe.

## UKIRI WA KINABII

**Kila wakati ninapoomba, kuna kusonga mbele katika roho yangu. Katika mwaka huu wa namna ya ki-Mungu, mafanikio yangu makubwa ya zamani yataonekana kama mchezo wa watoto. Ninaenda mbali zaidi ya kitu chochote nilichowahi kufanikiwa mpaka sasa kiasi kwamba shetani mwenyewe atashangaa.**

**SOMO LA ZIADA**
Habakuki 2: 1



**Ayubu 22: 23-25**
**Ukimrudia Mwenyezi, utajengwa; Ukiuondoa udhalimu mbali na hema yako. Nawe hazina zako ziweke mchangani, Na dhahabu ya Ofiri iweke kati ya mawe ya vijito; Naye Mwenyezi atakuwa hazina yako, Atakuwa ni fedha ya thamani kwako.**

Pesa inakuja kupima thamani. Na kuna thamani katika namna unayotoa, haswa, katika nia yako ya kutoa. Msingi wa kutoa ni kwa ajili Yake, sio kwa ajili yako. Ndio maana sio kila mtoaji atabarikiwa, na sio kila mtoa zaka atapokea. Mungu hatafuti mbegu ya pesa. Anatafuta mbegu ya moyo.

Malaki 3, aya ya 7 inasema kwamba nirudieni Mimi nami nitawarudia ninyi. Umekamata hiyo? Hasemi nitakurudi kama vile kurudi kwako. Hakuwahi kwenda kokote. Anasema kwamba moyo wako kumuelekea utakapobadilishwa, utatoa kwa nia sahihi, na aina hiyo ya kutoa itasababisha faida kukujia. Moyo wako utakapokuwa kwa ajili ya Ufalme, Mungu atakuwa kinga yako, na pesa zako zitalindwa. Kwa hivyo, unapaswa kufanya nini unapotoa? Badilisha mtazamo wako. Lengo lako linapokuwa Injili, utoaji wako unabadilika, na tuzo yako inabadilika. Weka moyo wako kumwelekea Yesu. Moyo wako utakapobadilishwa, utatoa dhahabu kama mavumbi.

## UKIRI WA KINABII

**Mbegu yangu inavuna roho, inajenga miji, inajali wajane na mayatima, na inapeleka Habari Njema ya Injili ulimwenguni kote. Mimi ni mtoaji mwenye nia ya Ufalme. Pesa yangu inalindwa, na faida ni hakika!**

**SOMO LA ZIADA**
Malaki 3: 7



## HAVE YOU RECEIVED JESUS CHRIST YET?

WE INVITE YOU TO MAKE JESUS CHRIST
THE LORD OF YOUR LIFE BY PRAYING THIS PRAYER;

"O LORD GOD, I COME TO YOU IN THE NAME OF JESUS CHRIST. I BELIEVE WITH ALL MY HEART IN JESUS CHRIST, SON OF THE LIVING GOD. I BELIEVE HE DIED FOR ME AND GOD RAISED HIM FROM THE DEAD. I BELIEVE HE'S ALIVE TODAY. I CONFESS WITH MY MOUTH THAT JESUS CHRIST IS THE LORD OF MY LIFE FROM THIS DAY. THROUGH HIM AND IN HIS NAME, I HAVE ETERNAL LIFE; I'M BORN AGAIN. THANK YOU LORD, FOR SAVING MY SOUL! I'M NOW A CHILD OF GOD. HALLELUIAH!"

CONGRATULATIONS! YOU ARE NOW A CHILD OF GOD.

TO RECEIVE MORE INFORMATION ON HOW YOU CAN GROW AS A CHRISTIAN, PLEASE GET IN TOUCH WITH US ON

UK: +44 3333 448 612
USA +1 240 781 6942
RSA +27 51 004 0209

WWW.UEBERTANGEL.ORG | WWW.GOODNEWSWORLD.COM

# SCRIPTURE PASSAGE FOR PROTECTION

## ISAIAH 54:

14 I AM BUILD SOLID, GROUNDED IN RIGHTEOUSNESS,
FAR FROM ANY TROUBLE—NOTHING TO FEAR!
FAR FROM TERROR—IT WON'T EVEN COME CLOSE!

15 IF ANYONE ATTACKS ME,
I WILL NOT THINK FOR A MOMENT THAT GOD SENT THEM,
AND IF ANY SHOULD ATTACK ME,
NOTHING WILL COME OF IT.

16 GOD CREATED THE BLACKSMITH
WHO FIRES UP HIS FORGE
AND MAKES A WEAPON DESIGNED TO KILL.
HE ALSO CREATED THE DESTROYER—

17 BUT NO WEAPON THAT CAN HURT ME
HAS EVER BEEN FORGED.
ANYONE WHO ACCUSES ME
WILL BE DISMISSED AS A LIAR.
I AM GOD'S SERVANT SO THIS IS WHAT I CAN EXPECT
GOD WILL SEE TO IT THAT EVERYTHING
WORKS OUT FOR THE BEST FOR ME."

THIS IS WHAT GOD SAYS TO ME AND
IT WILL NOT FAIL IN JESUS'S NAME!


TheGoodNewsWorld Helplines
USA: +1 (240) 781-6942
UK: +44 333 344 8612
RSA: +27 (51) 004-0209
www.goodnewsworld.com